# Nipashe

Ijumaa Oktoba 9, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580363

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ

nipasheTZ

0745 700710






**LISSU** atinga Mlimani, soko la Manzese

UKURASA 3

**MWALIMU** Mkuu matatani TAKUKURU tuhuma za udanganyifu wa mitihani

UKURASA 4

**WATANZANIA** milioni 2.4 wana matatizo ya macho, sababu zawekwa bayana

UKURASA 4

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### AJALI GARI YAKATISHA MAISHA YA HAKIMU

WATU wawili, akiwamo Hakimu Zakomeo Sanga...

UKURASA WA 4

### ONGEZEKO LA SARATANI KWA WASICHANA LATISHA

TAASISI ya Saratani Ocean Road (ORCI), imebainisha kuwapo ongezeko la saratani ya matiti kwa...

UKURASA WA 5

### SABABU MFUMUKO WA BEI KUPUNGUA

MFUMUKO wa bei wa Taifa kwa mwaka ulioishia Septemba, mwaka...

### Mume adaiwa kumpiga mke na fimbo hadi kufariki dunia

UKURASA 16

# Kada wa CHADEMA afanyiwa unyama

UKURASA 2



Rais John Magufuli na mgeni wake Rais wa Malawi, Dk. Lazarus McCarthy Chakwera, wakifunua pazia kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa kituo cha kisasa cha mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani cha Mbezi Luis, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# JPM aagiza mkandarasi kituo mabasi mikoani akatwe fedha

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA YAONGEZA 'DOZI' YA MAZOEZI UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6


Fursa kwa Wagombea! 2020

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE

HABARI KITAIFA

# JPM aagiza mkandarasi kituo mabasi mikoani kukatwa fedha

Na Christina Mwakangale

RAIS John Magufuli ameeleza kutoridhishwa na kasi ya ujenzi wa kituo cha mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani cha Mbezi Luis jijini Dar es Salaam na kuagiza mkandarasi wa mradi huo, kampuni ya Hainan International Limited ya China, kukatwa malipo yake.

Kituo hicho ambacho kilitakiwa kukamilika ujenzi Julai, mwaka huu, kimegharimu Sh. bilioni 71, lakini hadi sasa kimekamilika kwa asilimia 85.

Pia Rais alimwagiza Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo na Mkurugenzi wa Jiji, Sipora Liana kuhakikisha ujenzi unakamilika ifikapo Oktoba 30, mwaka huu.

Rais Magufuli aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uwekaji jiwe la msingi kwenye kituo hicho pamoja na Rais Lazarus Chakwera wa Malawi.

Licha ya kutokamilika kwa kituo hicho, pia alisema hajaridhishwa na ongezeko la gharama za mradi huo kutoka Sh. bilioni 31 hadi Sh. bilioni 71.

Kutokana na ongezeko hilo, Rais aliagiza gharama hizo zifuatiliwe kwa karibu na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Bodi ya Usajili na Wahandisi (ERB) pamoja na mhandisi mshauri, Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU).

Pia Rais Magufuli aliagiza kituo hicho kuwa na ofisi ya uhamiaji, mgawanyo wa maegesho kwa ajili ya bajaji, pikipiki pamoja na eneo maalumu kwa mabasi ya ndani na nje ya nchi.

Kwa upande wake, Rais Chakwera alisema anamshukuru Rais Magufuli kwa kumpa fursa ya kuweka historia ya mafanikio ya Tanzania, huku akiipongeza serikali kwa kuboresha miundombinu ya wananchi.

"Natambua kuwa wananchi wa Malawi wanapenda kusafiri kuja Tanzania kufanya biashara na ndugu zao Watanzania, hivyo naamini ujenzi wa kituo hiki utasaidia biashara na kuleta ustawi wa wananchi," alisema.

Pia alimshukuru Rais Magufuli kwa kushirikiana na Malawi katika makubaliano ya shughuli za maendeleo na kwamba umefika wakati wa Afrika kushirikiana.

Awali, Jafo akizungumzia kuhusu mradi huo, alisema kituo hicho kina uwezo wa kuchukua mabasi 3,456 yaendayo mikoani na nchi jirani.

Alisema mradi huo umetoa ajira takribani 600 na kitakapoanza kazi kitaajiri watu 10,000 na matarajio ni kukusanya mapato ya Sh. bilioni 10.2 kwa mwaka.

Rais Chakwera aliondoka jana alasiri kurejea Malawi baada ya ziara ya siku mbili nchini.

# Lissu atinga Mlimani City, soko la Manzese

Na Romana Mallya

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, jana aliibukia soko la Manzese jijini Dar es Salaam na kupokelewa na mamia ya watu waliokuwapo.

Awali, Lissu alianzia kwenye maduka makubwa ya Mlimani City ambako alinunua baadhi ya bidhaa na kusalimiana na watu na wengine wakiomba kupiga naye picha.

Akiwa sokoni Manzese, Lissu alionekana akisalimiana na wamachinga wanaouza bidhaa mbalimbali zikiwamo nguo za mtumba, huku akizungumza nao.

Lissu alionekana akipimisha suruali ya mtumba sokoni hapo, huku baadhi ya watu wakishangilia ujio wake.

Juzi, Lissu alipanda usafiri wa mabasi ya mwendokasi kutoka Kinondoni "B" hadi Gerezani, Kariakoo na kuelekea soko kuu la vyakula Kariakoo ambako alifanya ununuzi wa bidhaa mbalimbali.

Baada ya kushuka kwenye mwendokasi, Lissu alisema hiyo ni mara yake ya kwanza kupanda tangu mradi huo wa usafirishaji wa abiria uanze kutekelezwa jijini Dar es Salaam.

Pia, alisema ili mradi huo uwe bora zaidi, unatakiwa kuwa mfumo wa usafirishaji mkuu wa Dar es Salaam.

Lissu alishauri kwamba Dar es Salaam iko kwenye ukanda wa Bahari ya Hindi, hivyo inaweza kutumia usafiri wa majini kwa kuwa na boti kutoka Bunju mpaka bandarini na Kigamboni hadi bandarini ili kutatua tatizo la msongamano wa magari barabarani.

Lissu alisema Jiji la Dar es Salaam lenye zaidi ya watu milioni tano, halina mahali ambako watu wanaweza kwenda kupumzika.




## Ongezeko la saratani kwa wasichana latisha

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Saratani Ocean Road (ORCI), imebainisha kuwapo ongezeko la saratani ya matiti kwa wasichana nchini, kunakochagizwa na matumizi holela ya vidonge vya uzazi wa mpango.

Imesema wasichana wenye umri kuanzia miaka 25 ndio kundi lililothibitika kuwa katika hatari hiyo, kutokana na kutumia vidonge hivyo kinyume cha taratibu.

Hayo yalielezwa jana na Daktari Bingwa wa Utafiti wa Saratani wa ORCI, Samuel Kandali, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu mwezi wa uelimishaji wa jamii kuhusu saratani ya matiti.

Alisema kuanzia mwaka jana idadi ya wagonjwa wanaopata saratani ni kuanzia miaka 25 hadi 54, tofauti na miaka ya 2008/9, ambapo walikuwa wakipokea wagonjwa wa kuanzia miaka 64.

"Hatujafanya utafiti kuhusu sababu za wasichana wadogo kupata saratani hii, isipokuwa sababu kuu ni matumizi ya vichocheo vya homoni za mwili aina ya dawa za uzazi mpango kwa wasichana wadogo," alisema Dk. Kandali.

Alieleza zaidi kuwa, suala hilo limebainishwa wazi na wanafunzi wa Chuo cha Ufundi cha Ufundi Stadi (VETA) Kipawa, ambao walikiri wazi kutumia vidonge hivyo bila kufuata ushauri wa daktari.

"Wanafunzi wamekiri wazi wanatumia vichocheo vya mwili, bila mpangilio wakati mwingine kutumia dawa (alizitaja kwa jina) mara nne kwa mwezi hali ambayo ni hatari kwa afya zao na tunaweza sema kuwa ni moja ya sababu za kupata saratani hii," alisema Dk. Kandali.

Aliwataka wasichana wadogo kuepuka matumizi ya vidonge vya uzazi wa mpango, bila kufuata ushauri wa daktari, ili kujinusuru na tatizo hilo.

Daktari huyo bingwa, pia alizitaka taasisi mbalimbali nchini kushirikiana kufanya tafiti kufahamu zaidi sababu za kuibuka kwa wimbi hilo la mabinti wadogo kupata saratani.

Kuhusu mwezi Oktoba wa kuhamasisha jamii kuhusu uelewa wa saratani, alisema jana walitoa mafunzo na kuwafanyia uchunguzi wa awamu, walimu na wanafunzi wa VETA Kipawa.

Alisema walifikia wanafunzi 300, walimu 30 na kufanya uchunguzi wa watu 25, ambao wote hawakubainika kuwa na tatizo hilo.

Dk. Kandali alisema waliwaeleza wanafunzi hao kuhusu visababishi vya saratani kuwa ni uvutaji tumbaku, unene uliokithiri na kutofanya mazoezi na kuwataka kubadili mfumo wa maisha kwa kuchangamsha mwili kwa mazoezi angalau nusu saa kila siku.

"Tunaendelea kutoa elimu kwa jamii kupitia vyombo vya habari kuyafikia makundi mbalimbali lengo ni kujenga uelewa kwa jamii hasa kuondokana na dhana potofu kuhusu ugonjwa huu," alisema Dk. Kandali.

Naye Kaimu Meneja Rasilimali Watu wa VETA Kipawa, Upendo Abraham, aliishukuru ORCI kwa kuwapa elimu hiyo, ambayo itawasaidia vijana kutambua visababishi, ili kuzuia kupata ugonjwa huo.

Alisema wanafunzi 124 na wafanyakazi 24 walikuwa tayari kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa awali, ili kugundua kama tayari kama wana ugonjwa huo waanze matibabu.

# Mwalimu mbaroni madai udanganyifu wa mitihani

**Na Jaliwason Jasson,** KITETO

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) katika Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara inamshikilia Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi ya Olkitikiti, Oscar Waluye, kwa tuhuma za kufanya udanganyifu katika mitihani ya taifa ya darasa la saba iliyomalizika jana.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Manyara, Holle Makungu, alithibitisha jana kukamatwa na kushikiliwa kwa ajili ya mahojiano.

Alisema Mwalimu Waluye ambaye kituo chake cha kazi ni Shule ya Msingi Olkitikiti iliyoko katika Kijiji cha Engong'ongawe, anadaiwa kuwalazimisha wanafunzi wa darasa la sita kufanya mitihani ya darasa la saba.

"Akiwa Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, anatuhumiwa kuwalazimisha wanafunzi wawili wa darasa la sita katika shule hiyo kufanya mitihani ya darasa la saba," alisema Makungu.

Kwa mujibu wa Makungu, wanafunzi hao walilazimishwa kufanya mitihani badala ya watahiniwa ambao uwezo wao darasani unaelezwa kuwa ni wa kiwango cha chini.

Waluye anatuhumiwa kufanya udanganyifu huo, kwa kumkaririsha mitihani hiyo mwanafunzi mmoja.

Aidha, taarifa hiyo ilieleza kuwa wanafunzi hao wawili wa darasa la sita na mwanafunzi aliyehitimu mwaka jana, walikamatwa na makachero wa TAKUKURU wakiwa tayari wameishafanya mitihani ya masomo ya Kiswahili na Hisabati kwa niaba ya wenzao wa darasa la saba.

"Uchunguzi wa shauri hili unaendelea na mara utakapokamilika hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mwalimu huyo," alisema.

Makungu aliwataka walimu wote nchini kufanya kazi zao kwa uadilifu kwa kuwalea watoto katika njia iwapasayo ikiwa ni pamoja na kusoma kwa bidii.



Mke wa Rais, Mama Janeth Magufuli na mke wa Rais wa Jamhuri ya Malawi, Mama Monica Chakwera wakipata maelezo kuhusu maonyesho ya urithi wa asili na utamaduni, walipotembelea Makumbusho ya Taifa na Jumba la Utamaduni, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: IKULU**

# Milioni 2.4 Tanzania wana matatizo ya macho

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ZAIDI ya watu milioni 2.4 nchini wana matatizo ya kuona huku ugonjwa wa kisukari ukitajwa kuwa miongoni mwa sababu kuu saba zinazochangia hali hiyo.

Kutokana na hali hiyo, serikali imeandaa mkakati mwingine wa kukabiliana na tatizo la macho unaotarajiwa kusogeza huduma za macho karibu na wananchi.

Mkurugenzi wa Tiba katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Grace Magembe, alisema jana kuwa takwimu zilizotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonyesha asilimia moja ya watu kwenye nchi zinazoendelea na za uchumi wa kati wana ulemavu wa kuona.

Dk. Magembe alikuwa akizungumza kwenye maadhimisho ya Siku ya Afya ya Macho Duniani huku akibainisha kuwa Tanzania kuna watu 600,000 wenye ulemavu wa kuona.

"Pia watu wenye matatizo ya kuona kwa kiwango cha kati na juu hapa nchini wanakadiriwa kuwa ni mara tatu ya watu wasioona ambao ni takribani watu milioni 1.8. kwa ujumla Tanzania ina watu milioni 2.4 wenye matatizo ya kuona," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema watu wanaokaa kwa muda mrefu kwenye runinga na komputa wako hatarini kupata upofu kutokana na mwanga wa vitu hivyo kuwa na athari.

Alitaja visababishi ambavyo vinaweza kuzuilika ni pamoja na upeo mdogo wa macho kuona au uoni hafifu unaorekebishika kwa miwani, mtoto wa jicho, shinikizo la jicho, makovu kwenye kioo cha mbele cha jicho, vikope, tatizo la retina linalotokana na ugonjwa wa kisukari.

Pia alisema upofu wa utotoni utokanao na upungufu wa Vitamin A, mtoto wa jicho, maambukizi ya surua, kisonono kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na saratani ya macho kwa watoto.

"Iwapo una tatizo la kisukari, hakikisha umefanyiwa uchunguzi maalum wa macho hata kama huna dalili yoyote na kufuata maelekezo ya daktari kwa kuwa ugonjwa huu una sababisha tatizo kwenye retina," alisema.

Mkurugenzi huyo alitaja hatua mbalimbali ambazo serikali imechukua kupambana na upovu unaozuilika kuwa ni kuongeza vituo vya kutolea huduma za afya ya macho kutoka asilimia 75 mwaka 2007 hadi kufikia asilimia 93.9 hivi sasa.

"Pia miundombinu imeboreshwa ya huduma za upasuaji wa macho kwenye hospitali za mikoa 26 nchini," alisema.

Alisema pia huduma za uchunguzi wa macho kwenye kliniki za kisukari zimeongezeka kutoka wagonjwa 14,000 mwaka 2017 hadi kufikia 22,000 mwaka 2019.

Akizungumzia mkakati mpya, Dk. Magembe alisema unalenga kuimarisha huduma za macho za msingi sambamba na kutoa huduma za afya ya msingi ngazi zote.

## Malipo mtandao yapunguza matumizi ya fedha taslimu

**Na Waandishi Wetu**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imesema matumizi ya njia mbadala za kidigitali kwenye malipo katika uchumi, badala ya fedha taslimu yameongezeka.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na BoT na Idara ya Uhusiano wa Umma na Itifaki, hali hiyo ni kutokana na utafiti uliohusu maendeleo ya matumizi ya njia mbadala za malipo katika uchumi badala ya pesa taslimu.

Taarifa hiyo ilisema hatua mbalimbali zilizochukuliwa kupunguza matumizi ya pesa taslimu katika kufanya miamala ni pamoja na maendeleo katika masoko ya fedha duniani kwa kuzingatia faida zinazoambatana na matumizi ya pesa katika uchumi.

BoT ilisema malipo ya kidijitali kwa ajili ya kupunguza gharama za utoaji wa huduma za fedha taslimu kwa watu wa kipato cha chini, yameongeza usalama na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa njia ya kupunguza gharama za kuchapisha , kutengeneza na kusambaza noti na sarafu.

"Hatua zilizochukuliwa kupunguza matumizi ya fedha ni pamoja na kutengeneza mifumo ya malipo ya kidijitali, ikiwamo mfumo wa malipo baina ya benki mfumo wa malipo wa Afrika Mashariki, mfumo wa malipo kwa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Jangwa la Sahara (SADC), mfumo wa kidigitali wa malipo ya hundi, mfumo wa kielektroniki wa kutumia fedha na matumizi zaidi ya malipo," ilisema.

Aidha, utafiti huo ulibaini kuwa hatua nyingine ni kutoa leseni kwa kampuni za simu ziweze kutoa huduma za kifedha kupitia simu za mkononi.

"Lengo la waraka wa benki kwa taasisi za fedha ni kuiwezesha BoT kukusanya taarifa zinazowezesha kufanya tathmini ya matokeo ya hatua zilizochukuliwa na kuamua hatua zaidi za kuchukua kisera, kisheria na kiteknolojia," ilisisitiza taarifa hiyo.

**Imeandikwa na Frank Maxmillian, (TUDARCo) na Betrina Bishubo (SJMC)**

## Sababu mfumuko wa bei kupungua

**Na Elizabeth Zaya**

MFUMUKO wa bei wa Taifa kwa mwaka unaoishia Septemba mwaka huu, umepungua hadi kufikia asilimia 3.1 kutoka asilimia 3.3 Agosti, huku sababu zikibainishwa. Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema hali hiyo inamaanisha kuwa kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka Septemba imepungua ikilinganishwa na kasi iliyokuwapo Agosti mwaka huu.

Dk. Chuwa alisema kupungua kwa mfumuko wa bei kumechangiwa na kupungua kwa bei za bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula kwa Septemba ikilinganishwa na ilivyokuwa kwa bei za Agosti.

Alitaja baadhi ya bidhaa zilizopungua bei ni mchele, asilimia 2.0, mahindi 10.2, unga wa ngano 1.3, mihogo 18.4, na viazi vitamu asilimia 10.7.

Bidhaa nyingine ambazo alisema zilizopungua bei ni mafuta ya taa, kwa asilimia 15.6, dizeli kwa asilimia 14.2 na petroli kwa asilimia 10.2.

Kwa upande wa bei ya bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa Septemba zilipungua kufikia hadi asilimia 3.4 kutoka asilimia 3.7 Agosti.

Akizungumzia hali ya mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika Mashariki, Dk. Chuwa alisema kwa Kenya kwa Septemba mwaka huu umepungua hadi asilimia 4.20 kutoka asilimia 4.36 Agosti.

Kwa upande wa Uganda, Dk. Chuwa alisema mfumuko wa bei umepungua hadi kufikia asilimia 4.5 kutoka 4.6 Agosti.

## Majaliwa: Kuchagua Rais si kwa ushabiki

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (CC-NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kassim Majaliwa, amesema suala la kuchagua mtu wa kuliongoza taifa ni muhimu na halihitaji ushabiki.

Kutokana na hali hiyo, amewataka wananchi wahakikishe ifikapo siku ya kupiga kura, wanachagua kiongozi madhubuti atakayewaletea maendeleo.

Majaliwa alitoa kauli hiyo jana alipozungumza kwa wakati tofauti na wakazi wa kata za Kikunde, Tunguli na Kwekivu, Kilindi mkoani Tanga katika mikutano ya kumwombea kura mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Dk. John Magufuli pamoja na mgombea ubunge wa jimbo la Kilindi, Omari Kigua na wagombea wa udiwani wa CCM.

"Tunatafuta viongozi wa kuliongoza taifa ambao ni Rais, wabunge na madiwani. nawaomba ifikapo Oktoba 28, mwaka huu, tujitokeze kwa wingi kwenda kumchagua mgombea wa urais wa CCM, Dk. John Magufuli, kwani ni kiongozi pekee atakayeweza kuwaongoza wananchi wote, bila ya kujali itikadi zao vyama vyao," alisema. Majaliwa alisema Magufuli ni kiongozi, ambaye ameingia katika nafasi hiyo si kwa majaribio bali ni mtu ambaye anajua na ana uwezo wa kuwatumikia wananchi na mfano ameuonyesha katika kipindi cha miaka mitano ya awali ambayo ameongoza taifa kwa mafanikio makubwa. "Ombi hili ni kwa Watanzania wote haliangalii wewe ni wa chama gani. Halina ushabiki, nawaomba wote tukamchagüe Dk. Magufuli kwa nafasi ya urais, wabunge na madiwani wa CCM nchini kote, ili washirikiane kuwaletea maendeleo. Nawaomba mwendelee kuwa na imani na serikali ya CCM kwani imedhamiria kuwatumikia," alisema.

BIASHARA ZOTE MAKINI
HUTANGAZWA HAPA
Nipashe Nipashe mwendo mdundo
Unafahamu ni kwa nini?
"Tunaongoza na Kuaminika"




Nipashe MWANGA WA JAMII
WASILIANA NASI
0745 700 710 au 0677 020 701
advertise@guardian.co.tz (Matangazo)
subscription@guardian.co.tz (Magazeti)
epaper@guardian.co.tz (epaper)
PATA NAKALA YAKO
https://epaper.ippmedia.com
Pakua The Guardian-IPP Media
App Store Google Play
KUWA WA KWANZA KUHABARIKA
TUFUATE nipashetz nipashe TheGuardiantz YouTube TheGuardiantz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Fursa za ushirikiano Tanzania na Malawi zinufaishe pande zote

**MFUMO** wa uchumi wa dunia ya sasa unazitaka nchi kushirikiana ili kupaa kimaendeleo. Hali hiyo ni tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma hususan wakati wa vita baridi kati ya itikadi ya ujamaa na ubepari. Baada ya mfumo wa soko huria kushika kasi na kuyalazimisha mataifa yote kuufuata, sasa ushirikiano wa kiuchumi ndiyo imekuwa njia ya kila taifa kutumia kusonge mbele kiuchumi.

Mataifa yanayoendelea nayo yamejikuta yakilazimika kufuata njia hiyo kwa kuanzisha kanda mbalimbali za ushirikiano kwa mfano, nchi za Afrika zimekuwa zinaendelea kwa kasi kushirikiana kiuchumi kupitia jumuiya za SADC, ECOWAS, EAC, IGAD, COMESA, kwa kutaja baadhi.

Hii inamaanisha kwamba nchi zinaposhirikiana kikanda zinakuwa na nguvu ya pamoja kwa maana ya kuwa na soko kubwa sambamba na kugawana fursa zinazopatikana kila upande kupitia biashara. Ushirikiano wa kikanda kimsingi, umezinufaisha sana nchi za Afrika kwa sababu umeziwezesha kutegemeana kwa njia mbalimbali, ikiwamo kutekeleza miradi mikubwa kadhaa inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo kwa pamoja.

Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa ushirikiano wa mataifa ya Afrika kupitia kanda ni muhimu na uendelee kwa kuwa unaonyesha kwa vitendo kwamba unaweza kuziendeleza nchi hizo kiuchumi na kuwaletea wananchi wake maendeleo.

Tumeligusia jambo hili na kulipa msisitizo wakati huu ambao Rais wa Malawi, Dk. Lazarus Chakwera, amefanya ziara ya siku mbili ya kiserikali nchini kuanzia juzi na kumalizika jana, huku mataifa hayo jirani na wanachama wa SADC yakifikia makubaliano kadhaa ya ushirikiano. Juzi katika siku ya kwanza ya ziara ya kiongozi huyo, Tanzania na Malawi zilikubaliana kushirikiana kuboresha sekta za usafirishaji, uvuvi, madini, utalii na kilimo. Makubaliano hayo yalitangazwa juzi Ikulu jijini Dar es Salaam katika hafla maalum iliyohusisha marais Dk. John Magufuli na mgeni wake, Dk. Chakwera.

Rais Magufuli alimshukuru Rais Chakwera kwa kuitembelea Tanzania na kuwa nchi tatu kutembelewa, barani Afrika, baada ya Burundi, Uganda tangu aingie madarakani.

Aidha Rais Magufuli alielezea kuwa nchi hizo mbili zina historia ya undugu kutokana na muingiliano wa watu wake katika shughuli mbalimbali ikiwamo biashara kati ya mataifa hayo ambayo inaelezwa kupanda. Rais Magufuli alisema ilikadiriwa kuwa Dola za Kimarekani milioni 60 mwaka 2015 hadi miloni 80 hadi 81, na kwamba nia ni kutaka biashara ipande zaidi.

Pamoja na makubaliano yaliyofikiwa kwenye sekta kadhaa, bado tunaona kwamba Tanzania na Malawi zina maeneo kadhaa na fursa za kushirikiana kwa lengo la kuharakisha maendeleo ya wananchi wa mataifa hayo. Malawi ina fursa ya kuzitumia bandari za Dar es Salaam na Mtwara kutokana na umbali mfupi uliopo na kwa gharama nafuu ikilinganishwa na bandari za nchi zingine.

Hii ndiyo sababu iliyomfanya Rais Magufuli kusema juzi kwamba watu wa Malawi wasijihesabu kama nchi yao haina bahari, badala yake wajione wana bandari zake za Mtwara na Dar es Salam.

Kwa upande wake, Tanzania inanufaika na Malawi kwani kuna kampuni nane za uwekezaji ambazo zimeajiri zaidi ya Watanzania 390, na kwa upande mwingine zipo kampuni zilizowekeza Malawi kutoka nchini.

Aidha Rais Magufuli alisisitiza kuwa usafiri ukiimarika utafanya biashara ifanyike kwa urahisi, hivyo nchi hizo mbili zijiikite kwenye mahusiano ya kibiashara tu.

Rais Chakwera alisema ushirikiano utarahisisha usafiri wa haraka kupitia bandari ya Dar es Salaam na Mtwara kusafirisha mizigo yao hadi bandari ya Malawi.

Tunaamini kuwa kuwa makubaliano hayo yatatekelezwa kama ilivyopangwa na kwa wakati mwafaka, lakini jambo la msingi ni kuhakikisha kwamba fursa hizo zinanufaisha pande zote kiuchumi na maendeleo ya wananchi wake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kusoma ngazi moja, lakini matumizi ni muhimu zaidi

Na Ester Mgidula, UDSM

**KUNA** dhana ya elimu na kusoma. Mtu anaweza, ingawa anaweza akajiuliza na kutaka kufahamu aina gani ya usomaji unaozungumziwa hapa?

Hebu tujiulize maswali kadhaa, kama ni kwanini watu wanasoma shuleni, nini madhara ya kukosa fursa ya kusoma?

Pia, kuna uhusiano gani kati ya uchumi na elimu. Je, kila tajiri ameenda shule au kile anayefanikiwa aliipatia darasani?

Maswali hayo na mengine mengi yanaweza kupatiwa ufumbuzi, endapo tu mtu atajua umuhimu wa elimu na inaweza kufasiliwa kuwa ni ufahamu au maarifa ayapatayo mtu, ikipitia kutoka moja hadi nyingine.

Tuzungumze kidogo kuhusu elimu ya Tanzania, ambayo imegawanyika katika vipindi vitatu; kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya hapo kwa maana ya hadi sasa.

Kabla ya ukoloni elimu iliyotolewa ilihusisha zaidi ni ya vitendo, watu walifunzwa namna mfumo mzima wa maisha ulivyo, pia elimu kipindi hicho haikuhusisha maandishi kwa kina.

Wakati wa ukoloni, elimu ilitolewa na wageni mbalimbali kutoka nje. Wageni wa kwanza kufika Tanzania walikuwa Waarabu, wakifuatiwa na Wareno, Wajerumani kisha Waingereza.

Kutokana na kupokezana huko kwa utawala kwa baadhi ya maeneo au nchi nzima, kila kundi lilibadili mfumo wa elimu, mathalan katika mitaala na lugha ya kufundishia.

Vilevile malengo yake yalitazama matakwa yao, pasipo kujali manufaa kwa Watanzania. Lengo kubwa ililikuwa kupata watumishi wasaidizi ambao wangetumika kutetea matakwa ya wakoloni.

Kwa kipindi chao elimu iliyotolewa iliegemea nadharia zaidi. Mfumo huo wa elimu umeleta athari kubwa kwenye elimu, baada ya wageni kuondoka.

Baada ya Ukoloni, elimu iliendelea kuwa zaidi katika ngazi ya chini, ikiwamo kusoma na kuandika.

Kwa kiasi kidogo sana ilihusisha vitendo na mpaka sasa imebaki kuwa hivyo. Hapa ndipo panapoibuka mjadala kuwa, kusoma ni ngazi ya kwanza, lakini matumizi ya kilichosomwa ni ngazi muhimu.

Hivi sasa wasomi wamekuwa wengi na kila msomi anaamini kutendea kazi usomi wake kwa kupata ajira baada ya kuhitimu.

Fikra hizi ni za kizamani sana, kwa hali ilivyo sasa dunia haihitaji hivyo, bali elimu itolewayo itumike kwa vitendo. Maana yake nini?

Elimu inatoa mwangaza wa kuwaongoza watu katika njia iliyo sahihi, kwa hiyo tofauti ya wasomi na ambao si wasomi inaibuka hapa, kutokana na namna wanavyoyoendesha maisha yao, endapo mtu atakosa elimu hatakuwa na uwezo wa kutenda vizuri zaidi kama ambavyo angesoma kwanza.

Vijana wengi wamekuwa wakizua mijadala mingi kuhusu matajiri waliofanikiwa bila kusoma, mwisho wa mijadala ni kuona hakuna maana yoyote kusoma, huku wakisahau kuwa hata tajiri huyo anasaidiwa kuendesha mali zake na waliosoma na ndiyo maana huajiri wasomi.

Kwa hapa Tanzania, serikali imekuwa ikisisitiza sana juu ya uchumi wa viwanda, suala ambalo utekelezaji wake hauendani na idadi kubwa ya wasomi waliopo kutokana na mfumo wa elimu ulivyo.

Sababu kuu ni kwamba unaegemea zaidi nadharia kuliko vitendo jambo linalopelekea kukosekana uzoefu. Siyo hivyo tu, bali hata katika fani nyinginezo, haitoshangaza wataalamu katika hatua ya awali wana ufanisi mdogo kutokana na ukosefu wa masomo yanayohusisha vitendo zaidi.

Ni vyema serikali ikalitambua hilo na kubadili mfumo wa elimu, utakaoboresha wasomi na kupanua soko la ajira, ili wasomi waanze kuzalisha vitu kwa ubora zaidi.

Kwahiyo, Kila mmoja afanye jitihada kutafuta elimu yenye manufaa, ili kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Elimu inaweza kuwa na faida nyingine kama kuwa njia bora ya kujenga taifa imara, kuongeza upeo au uwezo wa kufikiri kwa wanadamu, vilevile ni nyenzo muhimu kutatua matatizo katika jamii.

Aidha, tufahamu kuwa elimu haiwezi kuhamishika, kwa maana kwamba leo unaweza kupata elimu halafu kesho ikapotea kichwani kwa mtu, hivyo kusoma ni bora zaidi. Alamsiki.

HABARI KITAIFA

# Wahamiaji haramu wakutwa kanisani

Na Richard Makore, MWANZA

IDARA ya Uhamiaji mkoani Mwanza imewakamata viongozi saba wa kanisa la TGMIT maarufu kama kanisa la baba God na watu 24, ambao ni raia wa kigeni kutoka nchi za Rwanda na Burundi walioingia nchini kinyume cha utaratibu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Mwanza, Bahati Mwaifuge alisema, wahamiaji hao walikamatwa eneo la Kangae Manispaa ya Ilemela.

Alisema kanisa hilo linahusika kuwahifadhi wahamiaji hao badala ya kutoa taarifa kwa vyombo vya usalama, ili wakamatwe.

Kanisa hilo linalosadikiwa kuwa na waumini zaidi ya 2,000, limedaiwa kuwahifadhi wahamiaji hao wanaotoka nchi za Burundi na Rwanda.

Mmoja wa wananchi walioshuhudia sakata hilo, Gabriel Mbando, alisema ameshangaa kukuta ndugu yake aliyepotea mwaka mmoja uliopita akiwa kwenye kanisa hilo.

Kutokana na sakata hilo, Mwaifuge alitoa rai kwa wananchi kuwafichua watu wasiowajua ama kuwahisi kuwa siyo raia wa nchini.

Alisema kuwa kwa kufanya hivyo kutasaidia kukamata wahamiaji, ambao wakati mwingine hufanya vitendo vya uhalifu.



Mkurugenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), Paul Rwegasha (kushoto) na Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja Vodacom Tanzania Plc, Harriet Lwakatare, wakikata utepe kuzindua duka jipya la kisasa lililopo kwenye uwanja mpya (Termial 3), jijini Dar es Salaam jana, ikiwa sehemu ya maadhimisho ya sherehe za miaka 20 ya Vodacom nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# OSHA yapunguza ajali sehemu kazi

Na Frank Monyo

MKUU wa Wilaya ya Mkuranga, Filbert Sanga, amesema ukaguzi na elimu inayotolewa na Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), vimechangia kupunguza ajali sehemu za wilayani humo.

Sanga alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, alipofanya ziara katika ofisi za OSHA kujifunza inavyotekeleza majukumu yake ya kulinda afya ya mfanyakazi pamoja na mali za wawekezaji ili kuleta tija katika uzalishaji.

"Nianze kupongeza kazi kubwa mnazozifanya ambazo zimeleta mabadiliko makubwa sana katika sehemu nyingi za kazi. Huko nyuma kabla ya uwepo na maboresho kwenye taasisi hii ajali zilikuwa nyingi sana katika maeneo ya kazi na wafanyakazi wengi sana walikuwa wanapata ulemavu,"alisema.

"Lakini kwasasa baada ya kutoa elimu, maelekezo na ushauri na baada ya kuwa karibu na wenye viwanda na wafanyakazi, ajali zimepunguwa kwa kiwango kikubwa sana na wenyewe wamejua sasa umuhimu wa kuzingatia ushauri na maelekezo yanayotolewa na Mamlaka," aliongeza Sanga.

Aidha, Mkuu huyo wa wilaya alisema shughuli za kiuchumi ikiwemo viwanda zinakuwa kwa kasi katika wilaya yake hivyo kupelekea umuhimu wa ofisi yake kushirikiana kwa karibu na OSHA katika kulea shughuli hizo za kiuchumi ili ziweze kukuwa na kuleta tija.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alimshukuru mkuu wa wilaya huyo kwa kutambua mchango wa taasisi yake katika kuchochea maendeleo ya Wilaya ya Mkuranga na taifa kwa ujumla.

# Walio jirani hifadhi wataka elimu

Na Beatrice Shayo, aliyekuwa MBEYA

Wakazi wanaoishi katika vijiji vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha Kanda ya Kusini, wameomba kupatiwa elimu zaidi kuhusiana na masuala ya uhifadhi na wanyamapori, ili kumaliza migogoro kati ya wananchi na hifadhi.

Wameeleza kuwa elimu waliyonayo ni ndogo na baadhi ya wana vijiji hawana kabisa, jambo ambalo linasababisha kushindwa kutatua changamoto zinazohusiana na wanyamapori na uhifadhi.

Waliyasema hayo wakati wakihojiwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET) katika ziara iliyoandaliwa na Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID).

Akizungumza kwa niaba yao, Ofisa Mtendaji wa Kitongoji cha Mawindi, Edson Kilemile, alisema licha ya kuwapo na faida za kuwa karibu na hifadhi, bado wanachangamoto nyingi ikiwamo elimu haba katika uhifadhi wa wanyamapori.

Alisema kukosekana kwa elimu kumesababisha kuwapo na migogoro isiyo ya lazima.

Alisema baadhi ya wananchi wamejikuta wakiwakimbia watu wa sekta ya uhifadhi kutokana na mtazamo hasi waliokuwa nao, licha ya kwamba hawajafanya uhalifu wowote.

Naye Kamshna Msaidizi wa Hifadhi Kanda ya Kusini, Pius Mzimbe, alisema wana kitengo maalum cha ujirani mwema moja ya majukumu yake ni kutoa elimu ya masuala ya uhifadhi wa wanyapori na kuimarisha uhusiano kati ya wana vijiji wanaozunguka hifadhi.

Alisema elimu imekuwa ikitolewa kwa vijiji, japo baadhi ya wana vijiji hawaipi kipaumbele.

Alisema ofisi yake ina mikakati ya kuongeza nguvu kwenye elimu kwa wananchi, ili kuimarisha ushirikiano uliokuwepo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema baadhi ya wana vijiji wamekuwa wakitumia suala la elimu kama kisingizio cha kujilinda.

Alisema Halmashauri kwa kushirikana na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) walifanikiwa kupeleka wataalamu wanaohusiana na masuala mbalimbali ya sekta hiyo na kutoa elimu kwa wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi.

Mfune alisema mikakati iliyopo ni kuongeza nguvu katika kutoa elimu kwa wana vijiji, ili washiriki kikamilifu katika kutunza hifadhi hiyo.

Enabel

**Enabel – SAKIRP - Vacancy**

**Construction site supervisor - Kigoma region**

Enabel – the Belgian Development Agency is recruiting civil building technicians for the supervision of bridge construction works.

**Duty station:** Kigoma region Kakonko or Kibondo – willing to relocate in function of construction sites.
**Contract term:** 1 year extendable - competitive salary package(14 months' Salary i.e. Leave allowance and Christmas Bonus) Medical Insurance Coverage, Relocation allowance Etc.

**Profile:** minimum diploma in Civil Engineering or equivalent

**Experience:** minimum 2 years hands-on supervision of masons and contractors.
Computer literate and good reporting skills in English/ Kiswahili.
Details vacancy at: https://btctanzania.wordpress.com/
Submit your applications to: recruitment.tza@enabel.be

**Deadline: 20TH October 2020 at 15:00 HOURS**

**Only shortlisted candidates will be contacted.**

# Elimu sheria yasaidia watu kujua haki zao

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

ELIMU ya sheria iliyotolewa katika maeneo mbalimbali mjini hapa imeelezwa kupunguza malalamiko yaliyokuwa yakiwasilishwa katika kituo cha msaada wa kisheria (KPC) na wananchi wameanza kufahamu haki zao.

Hayo yalibainishwa jana mjini hapa na Mkurugenzi wa Kituo hicho, Catherine Mlenga, wakati akizungumza na mwandishi wa habari hii namna wanavyotoa huduma ya kisheria kwa wakazi wa mji huo na mafanikio waliyoyapata.

Mlenga alisema wamekuwa wakitoa elimu ya kisheria zaidi ya miaka 10, kwa wananchi kuielewa sheria ya ndoa, mirathi na ukatili wa kijinsia kutambua haki zao.

Alisema pamoja na elimu hiyo ya kisheria, pia kituo hicho kinatoa msaada wa kisheria bure kwa watu wote, viongozi wa kata, vikundi vya vikoba na wananchi wa kawaida.

Mkurugenzi huyo alisema mwaka 2017 elimu ya kisheria iliwafikia watu 5,143 na pia watu 583 wanaume 256 na wanawake 327, walifika katika kituo hicho kupata msaada wa kisheria huku malalamiko mengi yakiwa yameelekezwa upande wa kesi za ndoa na huduma za watoto.

Hata hivyo kupitia Elimu hiyo takwimu zinaonyesha kuwa mwaka 2019, wananchi waliofika kupata huduma hiyo walikuwa 140, pekee wanawake wakiwa 88 na wanaume 52, ambapo msaada zaidi ulikuwa unahitajika upande wa matunzo ya watoto.

Mkurugenzi huyo aliziomba taasisi za msaada wa kisheria kusaidiwa, ili wahitaji wa ambao ni wa kipato cha chini waweze kupata huduma za kisheria bure kwa wakati.

# Baadhi vituo vya afya vyakosa umeme

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

BAADHI ya vituo vya afya na zahanati maeneo ya vijijini katika Wilaya ya Uvinza, havina nishati ya umeme na kusababisha baadhi ya huduma za mama na mtoto zinazotegemea nishati hiyo kama upasuaji na uongezaji damu kutokufanyika.

Akielezea hali hiyo Mkuu wa wilaya hiyo, Mwanamvua Mrindoko, wakati Shirika la World Vision kupitia mradi wa Sustain Kigoma, likikabidhi mradi wa umeme wa jua katika kituo cha afya cha Kalya, alisema ukosekanaji wa nishati ya umeme una fifisha utolewaji wa huduma ya mama na mtoto na kuwataka wadau kushirikiana na serikali kutatua.

"Pamoja na kwamba umeme wa REA unaendelea kusambaa, lakini kuna maeneo katika wilaya ya Uvinza umeme ule haujafika," alisema Mrindoko.

Alisema awali alikuwa akipigiwa simu nyingi na wananchi wakilalamikia utolewaji wa huduma za afya katika kituo cha afya Kalya, lakini tangu serikali ifanye maboresho pamoja na mradi huo wa umeme, hakuna malalamiko ya huduma zitolewazo.

Meneja mradi wa Sustain Kigoma, Dorothea Sago, alisema mradi umelenga kuboresha huduma ya afya ya mama na mtoto kwa kuhakikisha vifo vitokanavyo na uzazi vinapungua kupitia uhamasishaji kwa wanajamii kutumia huduma bora za afya na uboreshaji wa miundombinu.

Sago alisema mfumo wa umeme wa jua katika kituo cha afya cha Kalya umegharimu zaidi ya Sh. milioni 124 na umewezesha utolewaji wa huduma za msingi kama utunzaji wa damu salama, chanjo, vituo kutumia vifaa vya kuchemsha vifaa vinavyotumiwa na mama na mtoto pamoja na upasuaji.

Anastazi Raymond, mkazi wa Kalya alisema, awali walilazimika kutumia gharama kubwa kukodi boti, ili kumsafirisha mjamzito anapohitaji huduma ya upasuaji kwa kuwa kutoka eneo hilo hadi iliko huduma miundombinu ya usafiri ni mibovu hasa wakati wa masika.

Alisema kuna wakati wajawazito walipoteza maisha wakiwa njiani kuelekea hospitali zenye huduma ya upasuaji au kuongeza damu huku kukiwa na matukio ya usafiri wa majini kuzama katika Ziwa Tanganyika, upepo unapozidi.




Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA), wakitengeneza bomba la mji lililopasuka katika eneo la Mbezi Luis, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TCRA yaita wanafunzi, walimu kujifunza teknolojia

**Na Frank Monyo**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imewataka wazazi, walimu na wamiliki wa shule kuwapeleka wanafunzi katika Makumbusho ya mamlaka hiyo, kujifunza vitu vinavyotumika kwenye mawasiliano kabla ya teknolojia.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano wa TCRA, Mabel Masasi, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, wakati wa maadhimisho ya huduma kwa wateja, alisema wamefungua dawati maalum la kupokea maoni ya wadau.

"Tunawakaribisha watu wengi waweze kutembelea makumbusho yetu ambayo yapo makao makuu ya TCRA kwa ajili ya kujifunza mambo mbalimbali kuhusu teknolojia ilipotoka na tunapokwenda na hakuna malipo yoyote kwa yeyote anayetaka kuja kujifunza," alibainisha Masasi.

Alizitaka shule mbalimbali kutumia fursa hiyo kwa kupeleka wanafunzi kujifunza, kwa kuwa kuna mabadiliko makubwa katika mawasiliano na teknolojia kwa ujumla. Pia alisema katika maadhimisho hayo watapokea maoni ya wananchi juu ya utoaji wa huduma kwa umma.

## TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

# MWITO WA KUTOA MAONI

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili. Pia Mamlaka inadhibiti Umeme na Maji Safi na Usafi wa Mazingira kwa kuhakikisha huduma zinazodhibitiwa zinapatikana kwa viwango vya ubora wa kutosha; kwa bei halisi; salama na kwa uhakika; na kwamba watoa huduma wanapata faida halali na stahiki kwenye vitega uchumi vyao.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha Sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Dotto Damian F. Bulunda - Ngoma A<br>S.L.P 44<br>Buchosa | Kijiji cha Ngoma A, Kata ya Igalula, Wilaya ya Sengerema, Mkoa wa Mwanza | Dotto Damian Bulunda<br>(Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 2. | Mazami Filling Station<br>S.L.P 344<br>Musoma | Kiwanja Namba 1 Eneo la Mmazami, Wilaya ya Butiama, Mkoa wa Mara | Mussa Bupine Machemba<br>(Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha mafuta |
| 3. | Katura Fuel Service Station<br>S.L.P 1388<br>Musoma | Kiwanja Na. 65 Kitalu 'B' Eneo la Baruti Kata ya Mwigobero Manispaa ya Musoma Mkoa wa Mara | Angelina Katura Dibogo<br>(Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 4. | Vincent Augustino Ngowi<br>S.L.P 67315<br>Dar es salaam | Kiwanja Namba. 1, Kitalu "R", Eneo la Himo, Kata ya Makuyuni, Wilaya ya Moshi Vijijini, Mkoa wa Kilimanjaro | Vincent Augustino Ngowi<br>(Mtanzanai) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 5. | Olasiti Investment Company Limited<br>S.L.P 10275<br>Arusha | Kiwanja Namba 46, Eneo la Olasiti, Halmashauri ya Jiji la Arusha, Mkoa wa Arusha | Innocent Simon Moshi<br>(Mtanzania) | Leseni ya uuzaji wa mafuta kwa jumla |
| 6. | Mnyenye General Supplies Limited<br>S.L.P 154<br>Karatu | Kijiji cha Kambi ya Simba, Kata ya Mbulumbulu, Wilaya ya Karatu, Mkoa wa Arusha | Jublate Gerson Mnyenye<br>(Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 7. | Mastermind Tobacco (T) Ltd<br>S.L.P 22352<br>Dar es salaam | Kiwanja Na. 94 & 95, Eneo la Pugu, Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es salaam | Aggrey Mtui (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 8. | Pmm Estates (2001) Ltd S.L.P 33790,<br>Dar es Salaam | Eneo la Vingunguti, Wilaya ya Ilala, Mkoa wa Dar es Salaam | Judith Mhina (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 9. | Insignia Ltd<br>S.L.P 71449<br>Dar es Salaam | Kiwanja Na. 110/111, Eneo la Pugu, Wilaya ya Temeke, Dar es salaam | Kishan Dhebar<br>(Raia wa Uingereza) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 10. | Yapi Merkezi Insaat Ve Sanayi Anonim Sirketi<br>S.L.P 79317<br>Dar es Salaam | Eneo la Ngerengere, Wilaya ya Morogoro Vijijini, Mkoa wa Morogoro | Gokalp Kahraman (Raia wa Uturuki) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 11. | Jefag Logistics (T) Limited<br>S.L.P 70329<br>Dar es Salaam | Kiwanja Na. 2005, Eneo la Kurasini, Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es salaam | Emmanuel Mallya<br>(Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 12. | Yapi Merkezi Insaat Ve Sanayi Anonim Sirketi<br>S.L.P 79317<br>Dar es Salaam | Kilosa, Mkoa wa Morogoro | Gokalp Kahraman (Raia wa Uturuki) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 13. | Mexons Energy Limited - Bunju<br>S.L.P 38001<br>Dar es Salaam | Kiwanja Na. 53, Kitalu '8', Eneo la Mabwepande, Wilaya ya Kinondoni, Dar es salaam | Mexon Sanga<br>(Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 14. | Oilcom (T) Ltd – Ungindoni Service Station<br>S.L.P 20831<br>Dar es Salaam | Kiwanja Na.1, Kitalu L, Eneo la Kibada Ungindoni, Wilaya Ya Kigamboni, Dar es alaam | Said Edha Nahdi<br>(Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 15. | Mayunga Tito Hezron<br>S.L.P 433<br>Kilombero | Kiwanja Na. KIB/SQ/898, Eneo la Kibaoni, Ifakara, Mkoa wa Morogoro | Mayunga Tito Hezron<br>(Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 16. | MSK Petrol<br>S.L.P 68087<br>Dar es salaam | Kiwanja Na.17, Eneo la Mapinga, Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani | Venance V. Msacky (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 17. | Rupeez Oil<br>S.L.P 84<br>Bunda | Kiwanja Na. 210, Kitalu G, Eneo la Vijibweni, Wilaya ya Kigamboni, Dar es salaam | Elias Henry Rupia<br>(Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa muombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Imetolewa na**

**Mkurugenzi Mkuu,**

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**

215937602

# Makamba aonya Watanzania uchaguzi wasifanye kamari

**Na Thobias Mwanakatwe**

MBUNGE wa mteule wa Jimbo la Bumbuli (CCM), January Makamba, amewaomba Watanzania wasicheze kamari katika kuchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa sababu suala la kuongoza nchi linahitaji umakini.

Alisema hayo juzi katika mwendelezo wa mikutano yake ya kampeni vijijini kutafuta kura za mgombea urais wa CCM na madiwani wa chama hicho uliofanyika katika kata ya Funta na Tamota jimbo hilo.

Makamba alisema mgombea urais kupitia CCM, Dk. John Magufulu ana maono ni mzoefu katika uongozi na anatoka kwenye chama ambacho kina Ilani, sera na mipango bora.

Kadhalika, alisema baadhi ya wagombea wa vyama vingine sifa zao ni uanaharakati na hawana uzoefu wa kuongoza nchi wao binafsi na vyama vyao.

Aliwataka wananchi ifikapo Oktoba 28, wasikengeuke kuchagua vyama vingine bali wamchague Dk. Magufuli kwa sababu ni mzoefu wa uongozi na anatoka kwenye chama chenye historia na uzoefu wa kuongoza nchi.

"Tunakubali kila mmoja ana sifa zake, lakini sifa ya kushika hatamu ya uongozi wa nchi na kuamarisha vyombo vya ulinzi na usalama vilinde amani, mipaka ya nchi na utulivu anayo Dk. Magufuli hivyo msicheze kamari, wala msikengeuke kuchagua siku ya uchaguzi itakapofika," alisema Makamba.

Alisema baadhi ya wagombea wanakatisha tamaa hata kuwasikiliza kwa sababu badala ya kuzungumzia sera, wao wanazungumza matusi na kejeli kwa Serikali ya CCM.



Madereva wa bodaboda wakisubiri taa ziwaruhusu kuendelea na safari, huku baadhi yao wakiwa wamevuka eneo la waenda kwa miguu katika makutano ya barabara ya Morogoro na Kawawa, eneo la Magomeni, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni kinyume na sheria za usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mpakistan mbaroni kwa kuingia nchini bila kibali

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

IDARA ya Uhamiaji mkoani Kagera, imemkamata raia wa Pakistan, Mohamed Tahil, kwa kosa la kuingia nchini kinyume cha taratibu za sheria, akitokea Uganda.

Kamishna Msaidizi wa idara hiyo mkoani humo, Hamza Shaban, alisema tukio hilo lilitokea jana baada ya kufanya upekuzi.

Shabani alisema, raia huyo wa Pakistan alipitia njia zisizo rasmi na kuingia nchini kwa kutumia mipaka isiyofahamika.

Alisema amekaa kwa muda wa miezi sita nchini Uganda na kushindwa kuondoka kutokana na kuwa na kizuizi cha ugonjwa wa corona (lockdown).

Alisema, aliingia mkoani hapo kwa kupatiwa taarifa na watu kuwa nchini Tanzania hakuna ugonjwa huo, na kutafuta namna ya kutoka Uganda kuingia Tanzania bila kufuata taratibu.

"Sheria yetu ya Uhamiaji kifungu cha 45, kifungu kidogo cha (A), huyu bwana kuingia na uwepo wake hapa ni kinyume cha sheria, tumeanza taratibu za kumfikisha mahakamani," alisema Shabani.

Kwa upande wake, raia huyo alipohojiwa na vyombo vya habari alisema aliingia nchini kwa sababu Uganda mipaka yake imefungwa.

Mwisho.

## Mgombea aahidi kuvalia njuga tatizo la maji

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

MGOMBEA udiwani Kata ya Itezi, Jimbo la Mbeya Mjini, mkoani hapa kupitia CCM, Sambwe Shitambala, amesema akipewa ridhaa ya kuchaguliwa Oktoba 28, atahakikisha anamaliza tatizo la uhaba wa maji na migogoro ya ardhi.

Akizungumza na wananchi katika mkutano wa kampeni uliofanyika katika soko dogo la Jerere, eneo la Uyole, mgombea huyo wa udiwani ambaye kitaaluma ni mwanasheria, alisema kata ya Itezi imekuwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji kwa muda mrefu.

"Niwe mkweli wananchi wenzangu tatizo la ukosefu wa maji katika kata ya Itezi jijini Mbeya limekuwa likininyima usingizi kama mwananchi wa kata hii na ndiyo maana nimeamua kugombea nafasi ya udiwani kupitia Chama Cha Mapinduzi," alisema Shitambala.

Vile vile, alisema akipewa ridhaa ya kuchaguliwa kuwa diwani katika kata hiyo atashirikiana na wananchi na viongozi wengine kutatua kero hiyo na kushughulikia migogoro ya ardhi ili imalizike.

Alisihi wananchi kuwachagua wagombea wa CCM kuanzia diwani, mbunge na rais, ili kurahisisha upatikanaji wa maendeleo katika kata, jimbo na nchi kwa ujumla.


Kuhusu tatizo la maji, alisema limekuwa likimkera kwa muda mrefu kutokana na wananchi kuingia gharama ya kupata huduma hiyo.

Alisema kabla ya kugombea nafasi hiyo, kwa taaluma yake ya uanasheria amekuwa mstari wa mbele kuwasaidia wananchi wa kata hiyo masuala ya kisheria kuhusu tatizo la migogoro ya ardhi.

Alisema kuna wananchi wanyonge wananyanyasika kuhusu migogoro ya ardhi kutokana na baadhi ya wenye fedha kuwahangaisha na kwamba amekuwa mstari wa mbele kuwatetea.

Pia, alisema atahakikisha anafuatilia kwa ukaribu tuhuma za uuzwaji wa maeneo ya shule na baadhi ya vigogo ndani ya kata hiyo.

Alisema atashirikiana na wananchi kujenga zahanati ndani ya kata hiyo, kuboresha masoko madogo ili kuwawezesha wananchi wa kawaida kukuza uchumi.



Ukurasa 13

Watoto wasihusishwe kwenye kampeni

BUFE

IJUMAA OKTOBA 9, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 14

**Kishindo cha corona kilivyotikisa biashara ya utalii na nyendo zake**

**Na Halfani Chusi**

# Lijue shirikisho linalovikusanya vikundi kuvijengea uwezo mpya

- Vimefikiwa 120, kinamama na vijana
- Ajenda mbele yao 'baibai umasikini'

MSINGI ulioko ni kwamba katika hali ya kawaida, kila mtu anahitaji mafanikio, lakini namna ya kuyafikia hayo ndiko kwenye kitendawili.

Hilo pia, likigeuzwa upande wa pili wa sarafu, umaskini unaonekana kuwa janga linalowatafuna hasa kina mama na vijana kwa jumla, msingi mkuu ni kukosa mafanikio.

Ujumla wa maudhui ya ntazamo huo, ndio kunakobeba mazingira yanayozua maswali, ni namna gani hili linawezekana? Kila mtu akitafuta jibu katika hilo, atagundua kuna hatua imechukuliwa ya kinamama wengi wamejiunga katika vikundi vya ujasiriamali.

Hapo wanakabiliwa na changamoto ya kukosa mtu, anayewaunganisha katika umoja unaotambuliwa na serikali, ili wafikiwe na fursa za mikopo na elimu ya ujasiriamali, ili kuwawekea wigo mpana wa kujikwamua kiuchumi.

Kwa mtazamo wa kawaida, Shirikisho la Vikundi vya Ujasiriamali Tanzania (SHIVUTA), ni sehemu ya mfano wa majibu yaliyobuniwa kuhudumia kinamama na vijana, wajikwamue kiuchumi na pengine kufikia malengo sahihi.

Ni umoja ulioanzishwa mwaka jana, ukiwa na lengo lake la kutoa elimu na kuviunganisha vikundi vya ujasiriamali kuwa katika umoja ikiwezekana nchi nzima, ili vikishaungana kuwa kitu kimoja, viweze kuwashawishi wadau wawekeze na kuwapa mikopo ya pamoja.

Mkurugenzi wa SHIVUTA, Andrew Paul, anasema alishanzisha ushawishi huo kwa muda mrefu ya kuviunganisha vikundi.

"Mpaka hivi sasa tumeshaviunganisha vikundi 120 katika umoja huu, lengo letu ni kutoa elimu ya ujasiriamali, kuwaunganisha na wadau katika kupata mikopo mikubwa isiyo na riba," anasema Paul.

Anaendelea:"Pamoja na kuwajengea uelewa juu ya kutengeneza miradi ya kikundi, ambao baada ya kuanza kufanya hivyo mpaka sasa kuna matokeo chanya kwa baadhi ya vikundi."

Paul anakitaja kikundi mfano ni cha Msongola Matumaini Vikoba Group, ambacho kwa sasa kimejiunga na umoja huo, ili kuweza kufikiwa na fursa zinazopatikana huko na anasema kabla ya kuanza kuwapa elimu wengi wao walikuwa na uelewa mdogo katika mambo ya biashara.



Mwenyekiti wa kikundi Cha Msongola Matumaini, Peter Chacha, akiwasilisha mada katika semina ya wanakikundi wanaomsikiliza, kuhusu kujiunga na Umoja wa Wanavikundi vya Ujasiriamali Tanzania (SHIVUTA). **PICHA: HALFANI CHUSI.**

**WALIOJIUNGA WAFUNGUKA**

Mwenyekiti wa kikundi Cha Msongola Matumaini Vikoba Group, Peter Chacha, anaeleza mafanikio waliopata baada ya kujiunga na umoja na kusema umewasaidia kwa kiasi kikubwa.

"Tangu kikundi hiko cha Msongola Vikoba Group kijiunge katika Umoja huu na sasa wameanza kupata njia za kujikwamua kielimu, kupitia walimu wetu akiwapo Mwalimu Ayubu.

"Huyo ni mwalimu nzuri sana katika masula ya elimu ya ujasiriamali, sasa naona wanakikundi kwa sasa wana mitazamo chanya juu ya kuweka miradi ya maendeleo, kama mnavyoona.

"Kwa sasa, wanatarajia kujenga ofisi kubwa kwa ajili ya (mashine) kusaga, kukoboa na kuuza nafaka, pia wamefungua mradi wa kukodisha viti na maturubai kwa watu mbalimbali wanapokuwa na sherehe, hii pesa yote inaingia katika mfuko wa kikundi"anaeleza.

**OFISA UWEZESHAJI**

Mwalimu Ayubu anasema ni hali ambayo hivi sasa imekuwa mvuto kwa Ofisa Maendeleo Uwezeshaji Kiuchumi Wananchi wa Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam, Asenga Georgia, akiandaa mikutano kwa ajili ya baadhi ya vikundi kujiunga.

Hapo vinatajwa vikundi kama vya ujasiriamali Kivule (Uvuki) na Asenga anaahidi serikali ngazi ya wilaya itakuwa bega kwa bega, kuhakikisha wanapata stahiki zote katika umoja wao

"Muda wote, milango ya ofisi yangu ipo wazi kwa kuwa kwa sasa mmejiunga katika umoja ambao unatambuliwa kiserikali na mimi nitakuwa pamoja nanyi, kuhakikisha mnapata kila hitaji.

"Serikali inapenda watu kama nyinyi na sio serikali tu, hata kampuni nyingine. Nimefurahi sana mna harakati za kuukataa umaskini kwa nguvu zote na huu ni mfano wa kuigwa na ninaomba wote mchangamkie fursa hii, itawasaidia sana mtapata mikopo kwa wakati na elimu ya ujasiriamali," anasema Ofisa Ustawi - Asenga.

BIASHARA

## SIDO & MAISHA YA UJASIRIAMALI

# Mhitimu kompyuta chuo kikuu ang'ara utengenezaji sabuni uliobeba mafanikio

- Katika safari kuu kumiliki kiwanda
- Alisaka ajira jeshi akakosa...kasahau
- Mafanikio hayakosi kasoro, ayataja...

**Na Zuwena Shame**

KUNA shida ya ajira katika jamii zilizoko na hata nje ya mipaka na katika hilo, ujasiriamali unatajwa kuwa mkombozi kwa wengi, hasa katika nchi zinazoendelea.

Hivi sasa wajasiriamali wengi wamekuwa wabunifu katika shughuli zao za kuwaingizia kipato na kubuni bidhaa au kazi mbalimbali, kutegemeana na kasi ya ukuaji teknolojia na masoko.

Wataalamu wa uchumi wanabeba tafsiri kwamba, ujasiriamali ni uthubutu wa kuanzisha kipya, kwa kufanya cha kujipatia faida.

Nchini Tanzania kuna changamoto ya ajira na vijana wengi wanamaliza masomo katika fani mbalimbali, wanaishia kuhangaika mitaani.

Ugumu mojawapo unaowakabili, unatajwa ni haja ya kuwapo uzoefu wa kufanya kazi za fani au taaluma kwa wastani wa miaka mitatu au zaidi.

Katika nchi za Magharibi kama za Ulaya na Marekani, waligundua vyema adha hiyo ya pengo la ajira takribani 1700 iliyopita, kwa kubuniwa ujasiriamali kwa dhumuni la kuwajengea vijana wanaohitimu vyuoni kuweza, wajiajiri na kuondokana na dhana nzima ya kuajiriwa ofisini.

Hivyo, ni namna bora ya kuweza kufikia maendeleo halisi katika mfumo unaozungukwa na jamii fulani.

Nchini hilo linafanywa na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO), lenye umri wa miaka 47 na matawi katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

Inachokifanya ni walengwa kunolewa wawe wabunifu na wanaojitegemea katika ujasiriamali, biashara ndogo, uzalishaji mdogo kuelekea milki ya viwanda.

**SOMO LA ALIYETHUBUTU**

Andrew Mpambazi (26), kijana kutoka mkoani Kigoma, mhitimu wa Digirii ya Sayansi ya Kompyuta kutoka Chuo Kikuu cha Dar es salaam (UDSM) mwaka jana, baada ya kukutana na shida ya ajira, amejitosa rasmi katika ujasiriamali.



Sehemu ya bidhaa sabuni alizozalisha mjasiriamali katika picha tofauti.

Anachozalisha ni sabuni za miche na vipande, kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ikiwamo kuogea kuosha vyombo na kufulia na zinatengenezwa kwa kutumia malighafi kama matunda na sabuni.

Mpambazi anasema uamuzi wa kuwa mjasirimali baada ya kumaliza chuo na kukaa nyumbani bila ya mafanikio ya ajira katika ofisi mbalimbali, ilimuingiza katika uamuzi mpya mgumu.

Awali alilenga kusaka ajira katika Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), baada ya kuhitimu mafunzo, lakini hakufanikiwa.

Mpambazi anaeleza kilichomvutia kuchagua kuwa mbunifu na mjasiriamali wa sabuni, ni pale alipoona uhitaji wa sabuni baada ya kupata mafunzo kutoka SIDO, kwao mkoani Kigoma.



Hata hivyo, anakiri haikuwa rahisi kwake kuanza shughuli hiyo na maisha mapya, akijiuliza maswali kama angeweza kufikia malengo yake ya kuanza kuzalisha sabuni, kwani vijana wamekuwa wakiishia njiani wakikata tamaa, baada ya kupata kukumbwa an ugumu wa namna mbalimbali, katika safari yao kujiajiri.

"Haikuwa rahisi kwa upande wangu, pia vijana wengi tunakuwa na roho ya kukata tamaa mwanzoni mwa kuanzisha biashara au kujiajiri, ila kwa kuwa nina moyo wa ujasiri, niliweza kujipa moyo kuwa 'nitaweza' kutengeneza sabuni za 'champ' na kufika mbali" anasimulia.

**ASIMAMA KIBIASHARA**

Mpambazi anatamba kwa sasa ameanza kupata wateja kutoka mikoa mbalimbali nchini, akiwa amesimama vyema katika uwezo wa kuzaliosha sabuni na wasaidizi vijana anaopeana hamasa nao, katika dhana nzima ya kujiairi.

Anasimulia kwamba, kutokana na uwezo wake mdogo sasa kimtaji, bado hana kiwanda maalumu cha uzalishaji wa bidhaa yake, sabuni, bali amekodisha fremu ya duka akilenga ndoto ya kumiliki kiwanda baadaye.



Mjasiriamali, Andrew Mpambazi, akiwa na bidhaa za ubunifu wake. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU.**

"Mimi ndio dereva wa hii shughuli yangu ya kutengeneza sabuni za 'Champ', ila ninao watu ambao huwa nawalipa wakati wa uzalishaji wapatao 10 na wengine wakati wa usambazaji kama mawakala wapatao watano na wote ni vijana, isipokuwa kwenye usambazaji ndio yupo mama mmoja wa makamo" anaeleza Mpambazi.

Kuhusu soko, Mpambazi anasifu kiwa ni nzuri sana kwa maana Tanzania nzima inahitaji sabuni na viwanda vilivyopo havitoshelezi mahitaji, hivyo bidhaa yake anaipenyeza kushika soko.

Pamoja na hayo, anasema kuna ushindani mkubwa kati ndani ya soko la sabuni nchini, hasa kutoka baadhi ya viwanda anavyovitaja viko tangu kabla zama za uhuru wa nchi mwaka 1961 na anasifu ubora wa bidhaa zake ndio unasaidia kutikisa soko, kunasaidia afike mbali.

Anawataja walengwa wake ni kinamama, japokuwa wanaume na watoto wenye umri zaidi ya miaka miotano nao wako katika orodha yake.

Mpambazi anasema, kinamama vijana ndio wateja wake wakubwa, kutokana na hulka yao ya kujipenda na wakati huo huo, ina sifa ya kusaidia kujikinga na magonjwa ya ngozi.

**MATARAJIO YALIVYO**

Kuhusu matarajio yake, msomi huyo mhitimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, anaeleza dira yake ya kumiliki kiwanda kikubwa kitakachoweza kuzalisha sabuni nyingi sana kukidhi matakwa ya hitaji la kifaifa na kufikia nchi jirani, wajivunie anachokieleza "sabuni kutoka kwa kijana wao."

Mpambazi anasema kutokana na mtaji mdogo na kukosekana uaminifu kutoka kwa baadhi ya wateja, humkwamisha shughuli zake kimtaji, hasa kutoka wateja wasio waaminifu wanaochukua sabuni kwa mkopo na hawalipi inavyostahili au kutoweka kabisa.

Anaeleza ni hatua inayomcheleweshа katika uzalishaji awamu nyingine, kwani huwa anapaswa kununua malighafi ya kutengenezea sabuni, ambazo nyingi zinapatikana katika nchi jirani, Burundi.

"Pia, wengine wanakudhulumu pesa zako kabisa, kwa maana nimewahi kudhulumiwa pesa taslimu kiasi cha milioni moja. Hii ilitokea baada ya kumpa wakala sabuni kwa ahadi ya kuchukua pesa wiki moja mbele. Nilipoenda kuchukua, nikamkuta amekimbia na duka halikuwa la kwake na mwenye duka hanitambui," anasimulia mkasa.


Hata hivyo, Mpambazi anatoa wito kwa vijana kupenda kujiajiri na kwa kufanya na kubuni biashara tofauti, maana ndio kuna maisha mazuri na ya furaha licha ya matatizo yake.

Vilevile, ana wito kwa serikali na wizara inayoshughulikia vijana nchini, kuwajali wajasasiriamali vijana na wadogo kwa kuwajengea uwezo wa mafunzo na kuwapa mikopo ya mitaji na vifaa mbalimbali vya biashara, ili kuongeza chachu miongoni mwao vijana kujiajiri, hata wakapunguza tatizo la ajira.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Watoto wasihusishwe kwenye kampeni





**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
jkulangwa@yahoo.com

HIVI sasa, karibu kila kona ya nchi imegubikwa na harakati za uchaguzi. Kuna mikusanyiko ya hapa na pale ya watu kutoka vyama mbalimbali vya siasa, wakihutubiwa na wagombea uongozi katika kada za urais, ubunge na udiwani.

Uchaguzi Mkuu unafanyika Oktoba 28, wenye sifa na wamejiandikisha kupiga kura watakuwa wanatekeleza haki yao ya kikatiba ya kujichagulia viongozi watakaowaongoza kwa miaka mitano mingine ijayo.

Hiyo ndiyo demokrasia tuliyojiwekea na kuikubali na tumekuwa tukiidumisha kwa takriban miaka 60 sasa na mambo yamekuwa yakianza na kumalizia salama, licha ya dosari ndogondogo za hapa na pale.

Tanzania imeendelea kuwa nchi ya amani na utulivu, pawapo uchaguzi au pasiwapo uchaguzi, ili mradi wananchi wameendelea kujifanyia shughuli zao na kujiletea maendeleo yao.

Kampeni zinafanyika kwa utulivu na amani, pia wagombea wanajinadi kwa ahadi kedekede na tambo za hapa na pale, huku Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ikifuatilia kwa karibu na kutoa maelekezo pale inapostahili.

Inajulikana kikatiba, ni nani na nani wanahohusika na mchakato huo, kwa maana wanaostahili kupigiwa kura na wanaostahili kupiga kura, wanaochaguliwa na wanaochagua. Kifupi, ni kwamba aliye na umri wa chini ya miaka 18 haruhusiwi kushiriki uchaguzi.

Kushiriki uchaguzi kunaanzia katika kujitokeza kuwania nafasi ya uongozi, pia kujiandikisha kupiga kura na hata kushiriki kampeni za uchaguzi. Je, inatekelezwa nchini mwetu?

Ndiyo, inatekelezwa katika kipengele cha kujiandikisha na kushiriki kupiga au kupigiwa kura, yaani kuchagua na kuchaguliwa. Siyo, katika kushiriki kampeni, ambako tumekuwa tukishuhudia matukio kadhaa ya watoto wenye umri wa chini ya miaka 18 wakishiriki.

Maeneo mengi katika mikutano ya hadhara inayohutubiwa na wagombea, watoto wa rika hilo wamekuwa wakionekana kushiriki, wengine moja wa moja, lakini wapo ambao hawajitambui.

Wapo ambao wamekuwa hata wakivishwa sare za vyama na kushiriki mikutano hiyo na hata wakati mwingine kunadi wagombea kwa nyimbo, ngonjera na matukio yanayohusu uchaguzi.

Kuna ambao wamekuwa wakijikuta wanavutika na burudani katika mikutano hiyo, za nyimbo, ngoma, muziki na kadhalika na kufika maeneo hayo na hakuna anayewazuia.

Hakuna anayewazuia, kwa sababu yapo madai kuwa hata baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakiondolewa madarasani na kurudishwa majumbani kubadili sare na kuvaa kiraia na kutakiwa kufika kwenye mikutano hiyo.

Nia ni wahusika wa chama au wagombea wenyewe kutaka kuonyesha kuwa na mvuto na hivyo ndiyo sababu wanapata 'nyomi' ya watu kwenye mikutano hiyo na kujiridhisha kuwa siku ya kupiga kura watajizolea nyingi.

Ni kujidanganya kwa idadi ya watu mikutanoni na hasa ambayo inahudhuriwa na watoto wenye umri mdogo, kwamba kutakuwapo uwezekano wa ushindi wa kishindo, ni kinyume chake kwa sababu ukatili wa kuwapora watoto hao fursa ya elimu.

Kwa bahati mbaya sana, Watanzania tu wepesi wa kusahau, hivi karibuni 'Kovidi' ilitufanya vibaya hata kusababisha shule kufungwa na wazazi kusikitishwa na janga hilo, lililokuwa nje ya uwezo wao.

Pamoja na kupoteza muda sana wakiwa majumbani bila ya masomo, huku baadhi yao wakiambulia masomo ya luninga, bado wazazi hao na pengine walimu, wamesahau na sasa kuachia watoto waende kwenye mikutano ya kampeni ambayo hatimaye hautawafanyisha, kwani hawatashiriki uchaguzi.

Kana kwamba hiyo haitoshi, watoto hao baadhi yao wamekuwa wakishiriki kusikiliza matusi na lugha zisizo za kistaarabu zilizokithiri ukakasi zikitolewa na baadhi ya wagombea, hivyo kuzimeza hivyo hivyo na kuziamini kwa kuwa tu zimetolewa na viongozi kadamnasi.

Kama viongozi tutashindwa kuliona hili, na kulichukulia hatua, je tunaomba uongozi gani kwa wananchi huku tukishindwa kutekeleza ya msingi na muhimu katika makuzi ya watoto wetu?

BIASHARA

KURUNZI LA ARUSHA & MANYARA...

# Kishindo cha corona kilivyotikisa biashara ya utalii na nyendo zake

**Na Salome Kitomari, aliyekuwa Babati**

MOJA ya eneo lililoathiriwa kwa kiasi kikubwa na ugonjwa wa COVID-19 au corona, ni sekta ya Utalii, inayotegemea zaidi wateja wageni, hasa kutoka nchi za Ulaya na Marekani, ambazo kwa kiasi kikubwa ndiyo waathirika wakubwa wa ugonjwa huo.

Tangu kugundulika ugonjwa huo mwishoni mwa Desemba mwaka jana nchini China, ulisambaa kwenye mataifa mengi duniani kiasi cha kusimamisha shughuli za utalii, zinazotegemewa kuliingizia taifa fedha za kigeni na kuchangia pato la taifa.

Moja ya eneo lilioathiriwa na COVID-19 ni ikolojia ya Manyara Tarangire, yenye ukubwa wa kilomita za mraba 35,000, ikijumuisha asilimia 90 ya eneo la mtawanyiko la Simanjiro, maeneo yaliyohifadhiwa na Jamii ya Burunge, Simanjiro, Randilen na Makame.

Aidha, linajumuisha ranchi ya Manyara, Ziwa Natroni maeneo yaliyohifadhiwa (Game Contral Area) ya Mtoambu, Lokosare, Kitwai na Simanjiro pamoja na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara, ambayo zinabeba asilimia 10 ya eneo husika.

Eneo hilo ni muhimu sana kutokana na utalii unaoliingizia taifa mamilioni ya fedha na kunufaisha jamii ya eneo hilo, ambayo inafanya shughuli za maendeleo kwa kutegemea utalii.

Mathalani, Hifadhi ya Jamii Burunge WMA yenye ukubwa wa kilomita za mraba 283 lililotolewa na vijiji 10 vya kata tatu za Nkaiti, Mwada na Magara, ni kati ya hifadhi hizo 16 nchini ambazo zipo hai na nyingine 16 zipo taabani.

Aidha, Hifadhi za Tarangire na Ziwa Manyara ni muhimu kwa taifa, kutokana na kuwa tegemeo la mapato kitaifa, kwa mlango wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA).

Burunge WMA hutegemea wageni kutoka nje ya nchi kutembelea na kulala kwenye hoteli zilizopo eneo hilo, ikiwamo utalii wa picha, unaosaidia jamii kuuza bidhaa zao wanazotengeneza na huduma.

Katibu wake, Benson Mwaise, anasema wana wawekezaji watano, anaowataja kuwa ni: Lake Burunge Tinted lodge, Maramboi Tinted Lodge, Yulea, Tarangire River Camp, Tarangire Ospuko lodge na EBN Hunting Safari wanaomiliki kitalu cha uwindaji.

"Asilimia 75 ya mapato yote yanatokana na utalii wa picha, mengine ni uwindaji wa kitalii na faini mbalimbali kwa anayekwenda kinyume. Pia, tuna wahisani ambao wanaisaidia WMA kupitia huduma za kijamii na nyinginezo," anafafanua.

**MAPATO MIAKA 12**

Mwaise anafafanua mapato yao yaliongezeka kutoka Sh. milioni 37 mwaka 2006/07; mwaka 2007/08 (Sh. milioni 75.2); mwaka 2008/09 (Sh. milioni 64.5); mwaka 2009/2010 (Sh. milioni 391.4); mwaka 2010/11 (Sh. milioni 473.7); mwaka 2012/13 (Sh. milioni 275.4); na 2013/14 (Sh. milioni 412.5.)

Aidha, katika mwaka 2014/15 (Sh. milioni 820.94); 2015/16 (Sh. milioni 795.3); mwaka 2016/17 (Sh. bilioni 1.3); mwaka 2017/18 (Sh. bilioni 2.8); mwaka 2018/19 (Sh. bilioni 2.2) na mwaka uliopo 2019/20 (Sh. bilioni 2.5).

Katibu huyo anafafanua kwamba katika mwaka 2018/19, yalitokea mabadiliko ya kanuni kwamba kupunguzwa fedha za mapato zinazobakishwa WMA, akifafanua kwamba imeshushwa kutoka asilimia 75 za awali, hadi asilimia 65 za sasa.

Pia, asilimia 35 zinazobaki zigawanywa kwa misingi, asilimia 25 inapelekwa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), asilimia 10 zilizobaki zinapewa Halmashuri ambayo ni Babati.

"Mgawanyo wa asilimia 65 nusu inabaki WMA kwa ajili ya uendeshaji na kwa mwaka huu, Sh. milioni 674.3 ambazo hulipa mishahara, kufanya matengenezo, kesi, mishahara, kodi za serikali na gharama nyinginezo, huku kiasi kama hicho kikienda kwenye vijiji," anasema.

**ATHARI ZILIVYO**

Anasema katika mwaka 2019/20 walikadiria kukusanya zaidi Sh. bilioni 2.5, lakini kuanzia Mach 13, mwaka huu mgawo unatarajiwa kuwa Sh. milioni 76 kwa kila kijiji na utateremka zaidi kutokana na ukweli kwa sasa hakuna wageni kutoka nje ya nchi.

Mwaka 2018/19 tulikusanya Sh. bilioni 2.2 na kila kijiji kilipata Sh. milioni 100.9, lakini kutokana na janga la corona mgawo utakuwa Sh. milioni 67.5 kwa kila kijiji mwanachama," anasema.

Mwaise anasema, baada ya vijiji kupata fedha hizo hutumia taratibu zake kuzitumia baada ya kuidhinishwa na mkutano mkuu wa kijiji, chini ya usimamizi wa halmashauri zao.

"WMA tunakusanya na kuiingiza katika misingi ya uendeshaji, hadi sasa kila kijiji kimeshapata Sh. milioni 446.7 kutoka mwaka 2006 hadi 2019 na zote zimefanya shughuli za maendeleo na vijiji vyetu vina ofisi nzuri tofauti na vijiji vinavyotegemea michango ya wananchi," anasema.

Anafafanua mapato ya jumla tangu kuanza kukusanya fedha ka miaka 12 iliyopita yalikuwa zaidi ya Sh. bilioni 8.9.

**RC & RAS WAONGEA**

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Iddi Kimanta anasema utalii ni sekta mama kwa uchumi wa nchi na mkoa waje umejipanga kupata wageni waliojifungia kutokana na corona.

Anasema, Watanzania nao ni watalii katika hifadhi zao, kutokana na nafasi walizo nazo na wakienda kwenye maeneo ya vivutio na kuchangia uchumi huo.

"Tuna changamoto hata kwa waongoza watalii kujua mtalii ni nani, bado watu wanafikiri ni lazima atoke nje ya nchi. Kwa sasa tumeshusha vyumba vya kulala hifadhini kutoka Sh. 700,000 hadi Sh. 250,000 na tumeleta chai za Kitanzania na hoteli ziajaa wazawa," anasema

Rai yake kwa jamii, ni kwamba itembelee vivutio vya vilivyopo na kuchangia uchumi wa nchi.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, anaitajka sekta utalii ina umuhimu wa kipekee kutokana na mkoa kuwa na idadi kubwa ya vivutio kitaifa na idadi kubwa ya wageni wanaoingia.

Anasema, kuna zaidi ya kampuni 600 zilizosajiliwa kwenye utalii na hotel za kitalii za hadi kiwango cha nyota tano, akitoa mfano wilaya ya Karatu pekee ina hoteli 57 zinachangia ukuaji uchumi na kutoa ajira kwa wananchi wengi.

"Tulivyopata tatizo la corona tuliyumba kwa kiasi kikubwa, kwa kuwa hoteli na 'loji' zilifungwa na Leopard Tours magari 600 yaliegeshwa. Huyu ni mmoja na mwingine amefunga maeneo 25 na wafanyakazi zaidi ya 700 wenye ajira za kudumu walisimamishwa.

"Bahati nzuri hadi sasa kumekuwa na jitihada za kitaifa na mkoa zilikuwa nzuri na tulipata wageni kutoka China, Israeli na mataifa mengine. Kwa sasa watalii wameendelea kuja nchini na si kwa kiasi cha zamani lakini wanakuja,"anaeleza.



Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, akitoa ufafanuzi kwa waandishi wa habari za mazingira (hawapo pichani),kuhusu hali ya utalii mkoani humo na athari zilizosababishwa na corona. **PICHA: SALOME KITOMARI.**



Sehemu ya kitega uchumi cha kitalii, Lake Burunge Tented Lodge, iilyoko Babati, Manyara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**



# Ujenzi tangi la maji kutoa uhakika huduma miaka 50

Na Augusta Njoji, DODOMA

SERIKALI imeanza ujenzi wa mradi mkubwa wa tangi la maji katika mji wa Chamwino lenye uwezo wa kuhifadhi lita milioni 2.5 litakalosaidia wananchi kuishi bila tatizo la huduma hiyo kwa miaka 50.

Mradi huo unagharimu Sh. milioni 998 na umeanza kutekelezwa Septemba mwaka huu na utakamilika ndani ya kipindi cha miezi sita.

Akizungumza na Nipashe, Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma (DUWASA), Kanda ya Chamwino, George Mwakamele, alisema mradi huo ukikamilika utahudumia wananchi zaidi ya 35,000 ambao watakuwa na uhakika wa maji.

"Katika mradi huu tunajenga tangi lenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni 2.5 na kukamilika kwa mradi huu sasa kutaifanya shida ya maji kuwa historia kwa kipindi cha miaka 50 ijayo," alisema.

Alisema kwa sasa visima vinne vya maji vimeunganishwa na vinawezesha watu 28,434 kupata maji na kukamilika kwa mradi huo kutafanya kuwapo na ongezeko la watu 35,000 watakaopata huduma ya maji safi na salama kwa uhakika.

"Mradi huu wa tangi hautawasaidia tu wananchi wa hapa Chamwino bali tutaweza kuunganisha mabomba na kufikisha maji katika mji wa serikali Mtumba na hivyo kuwezesha uwapo uhakika wa upatikanaji wa maji," alisema.

"Uwezo wa tangi hili utasaidia upatikanaji wa maji lita milioni 5,280,000 kwa siku, lakini hatuishii hapa baadaye tutaongeza kufunga visima sita ambavyo kwa sasa havitumiki na hivyo kuongeza idadi ya uzalishaji kwa siku kufikia lita milioni nane."

Mmoja wa wananchi wa eneo hilo, Jeni Mahindoni, aliishukuru serikali kwa kuanza ujenzi wa mradi huo ambao utafanya Chamwino tatizo la maji kuwa la kihistoria.

"Tulikuwa tunatumia muda mwingi kutafuta majisafi, wengine tulikuwa tunachota kwenye makorongo, lakini naamini mradi utakapokamilika tutaelekeza nguvu zetu kwenye shughuli za kujipatia kipato," alisema.



Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto kutoka Wizara ya Afya, Maenedeleo Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Ahmad Makuwani (katikati), akizungumza na viongozi mbalimbali wa dini mkoani Dodoma jana, wakati akifungua semina ya uelimishaji jamii kwenye makanisa na misikiti juu ya umuhimu wa kupatiwa chanjo. Kulia ni Meneja Mpango wa Taifa wa Chanjo, Dk. Dofrossa Lyomo na Kaimu Mganga Mkuu Jiji la Dodoma, Dk. Joseph Mdachi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Aagiza kituo kuzalisha mbegu bora

Na Augusta Njoji, DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, ameagiza uongozi wa Kituo cha Mafunzo ya Wakulima Bihawana jijini hapa, kuongeza maeneo kwa ajili ya kuanzisha mashamba makubwa ya kimkakati, ili kuzalisha mbegu bora.

Alitoa agizo hilo jana alipofanya ziara ya kutembelea kituo hicho ikiwa ni mwendelezo wake wa kukagua vyuo vya Mafunzo ya Kilimo (MATI's) vya Umma na pamoja na Vituo vya Mafunzo ya Wakulima (FTC). Aliwataka kuongeza maeneo hayo hata yakiwa mbali na kituo, ili kuzalisha mbegu bora au mazao ambayo yatauzwa na kuleta faida kwa kituo.

"Hizi ziara ninazofanya zina lengo la kujenga dhana ya kujitegemea ili kuleta mapinduzi ya kiuchumi kwa watumishi na wakulima nchini si kwa lengo la kufanya utalii," alisema.

Kadhalika, alisema anataka kuona miradi mingi ikianzishwa na kuwa mashamba ili mazao hayo yauzwe na fedha hizo zitumike kuendesha shughuli za usimamizi na maendeleo.

"Napenda pia mfikirie kuongeza maeneo kwa ajili ya kuwekeza na muwe mkiongea na viongozi wa vijiji au mitaa, kuwaomba maeneo makubwa kwa ajili ya kuongeza tija na faida katika kilimo," alisema.

Katika ziara yake, Kusaya alitoa ng'ombe wakubwa wawili, vifaranga vya kuku 1,000 kwa ajili ya kuanzisha mradi mkubwa wa ufugaji pamoja na kutoa Sh. milioni 10 kama sehemu ya mtaji wa kuanzisha miradi ya kujenga dhana ya kujitegemea na kujiendesha kwa faida.

Pia, alimkabidhi Mkuu wa Kituo hicho, Emmanuel Mtenga pikipiki moja kwa ajili ya kuongeza ufanisi kwa utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

# Mavunde aahidi kuinua vikundi kiuchumi

Na Augusta Njoji, DODOMA

MGOMBEA ubunge kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, amesema akichaguliwa tena kuongoza jimbo hilo, ataviinua kiuchumi vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kuhakikisha fedha zinazotolewa na halmashauri asilimia 10 inawafikia.

Mavunde aliyasema hayo juzi kwenye mkutano wa kampeni katika Kata ya Tambukareli, jijini hapa.

Alisema kwa miaka mitano iliyopita amefanya jitihada za kuinua vikundi hivyo kupitia fedha za mfuko wa jimbo na ataendelea kusimamia hilo na fedha zinazotolewa na halmashauri.

Aliahidi kujenga mtandao wa barabara katika kata hiyo ikiwamo Kilimo kwanza hadi Makulu kwa kiwango cha lami, itakayoanza ujenzi wake hivi karibuni.

"Dodoma tunaongoza kwa kuwa na mtandao mkubwa wa barabara za lami kwa kilometa 169, nitaendelea kuhakikisha tunaongeza zaidi ili wananchi mpite kwenye lami na kuondokana na barabara za vumbi," alisema.

Alisema mwaka 2015 aliahidi ujenzi wa kivuko na sasa ujenzi huo umekamilika na wananchi hawapati tena kero hiyo.

"Kivuko kipo au hakipo? Mkinichagua tena kwa miaka mitano mbali na kutatua tatizo la miundombinu kwenye shule ya msingi Medelii, tunajenga madarasa 10 na hali ya mazingira kwenye hii shule yetu itaendelea kubadilika," alisema.

Pia aliahidi kuendelea na ujenzi wa kituo cha afya ambacho tayari ujenzi wake upo hatua ya msingi na awamu ijayo atahakikisha kinakamilika kujengwa.

"Katika ujenzi wa soko tumeomba fedha naomba mnirudishie diwani (Juma Mazengo), ili tukamilishe kuomba fedha kwa ajili ya kumalizia soko letu na pia nitashughulikia wananchi wanaodai fidia waliopisha eneo la shule wanalipwa," alisema.

Naye mgombea udiwani wa chama hicho, Kata ya Tambukareli, Juma Mazengo, aliwaomba wananchi wamchague ili kuwaletea maendeleo ikiwamo kutatua kero ya barabara.

"Mlikuwa hamna kivuko katika miaka yangu mitano iliyopita nimehakikisha kimewekwa na hatua hii imeondoa lile tatizo sugu ambalo wakati wa msimu wa mvua wananchi walikuwa wanashindwa kuvuka upande wa pili," alisema.

Alisema wakati anachaguliwa kwenye Shule ya Msingi Medelii wanafunzi walikuwa wanakaa chini na kutafuta zaidi ya Sh. milioni 100 ambazo zimetumika kununua madawati, kukarabati madarasa na ujenzi wa baadhi ya miundombinu, hivyo akawaomba wananchi wamchague tena ili akamilishe kutatua kero kwenye maeneo mengine.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Dodoma, Meja mstaafu Risasi Saringo, aliwahimiza wananchi kujitokeza Oktoba 28, mwaka huu, kupiga kura ili kuchagua viongozi bora wanaotokana na chama hicho.

"Tunzeni vizuri vitambulisho vya kupigiakura msije mkaenda kutumia vya NIDA (Kitambulisho cha Taifa), havitakiwi vinavyotakiwa siku ya kupiga kura ni vya kura ambavyo vimetolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), na msije mkaenda na sare za chama, mkifika pigeni kura kwa wagombea wa CCM yaani rais, mbunge na diwani," alisema.





# Tiba asili watakiwa kusajili huduma zao

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WATAALAMU wa tiba za asili katika Mkoa wa Mbeya, wametakiwa kusajili huduma zao, ili watambulike kwa mujibu wa sheria na kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria yanapotokea matatizo kwenye huduma hizo.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyatta, alisema hayo alipokuwa akizungumza na Nipashe kuwa takwimu zinaonyesha zaidi ya watoa huduma 3,000 hawajasajiliwa katika mkoa huo.

Alisema serikali imeweka utaratibu wa kusajili shughuli hizo ili zitambulike na kurasimishwa na zitumike kama ilivyo kwenye mataifa mengine ambayo zipo hospitali zinazotoa huduma kwa kutumia mitishamba.

Alisema huduma hizo ni kama maduka ya dawa za binadamu ambayo hayawezi kufanya kazi bila kusajiliwa na kuwasisitiza wataalamu wa huduma hizo kuzingatia sheria za nchi, ili kuepuka kushughulikiwa.

"Mnatakiwa mhamasishane wenyewe kujisajili, ukiona mwenzio anatoa huduma bila kusajiliwa ujuwe anakuharibia na wewe kazi yako, sasa utaratibu uko wazi na ni rahisi kabisa, naomba sana mjitahidi ili kazi zenu zitambulike na zikuwe," alisema Dk. Manyata.

Vile vile, alisema utaratibu wa kusajili huduma hizo unaanzia katika ofisi za maofisa watendaji wa mitaa na kata mpaka katika ngazi ya wilaya ambako ndiko vibali vinatolewa na kwa sasa huduma hizo zinafanyika kielektroniki.

Dk. Manyatta alisema mtoa huduma akishasajiliwa anatembelewa na maofisa wa halmashauri wanaokagua ubora wa huduma na mazingira ya kutolea huduma.

# Mbaroni tuhuma za kuua mke kwa kumcharaza fimbo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linamshikilia Samson Kyando (26), mkazi wa Kata ya Mswisi, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya kwa tuhuma za kumuua kwa kumpiga na fimbo sehemu mbalimbali za mwili mke wake Cecilia Wilson (24).

Imedaiwa kuwa chanzo na tukio hilo ni ugomvi wa kifamilia uliozuka baina ya marehemu na mtuhumiwa na kusababisha vipigo. Kwa mujibu wa Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Mbeya, Ulrich Matei, tukio hilo lilitokea Oktoba 4, mwaka huu baada ya mtuhumiwa kumshambulia mke wake Cecilia kwa kumpiga na fimbo sehemu mbalimbali za mwili na kumsababishia majeraha na kupelekwa hospitali ya misheni Chimala kwa matibabu. Matei alisema, Cecilia aliendelea kupatiwa matibabu na hadi kufikia Oktoba 6, majira ya saa nne usiku alipoteza maisha wakati madaktari na waduhumu wengine wa afya wakiendelea na jitihada za kuokoa uhai wake.

Kutokana na hali hiyo Jeshi la Polisi lilimtia nguvuni mtuhumiwa na upelelezi wa shauri hilo unaendelea.

Alitoa wito kwa jamii kushirikisha matatizo yao ili kuwa njia ya kumweka mtu kwenye usalama zaidi kuliko kufanya uamuzi wa hasira.

Katika hatua nyingine Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, linamshikilia Salome Buya (23), mkazi wa Mnazi kwa Ndomba, wilayani Mbarali kwa tuhuma za kumjeruhi shingoni Tabia Abdalah (38).

Tukio hili lilitokea Oktoba 6, saa 12 jioni katika Kijiji cha Mnazi, Kata ya Imalilosongwe baada ya mtuhumiwa kumjeruhi kwa kumchoma kisu shingoni Tabia Abdalah na kusababisha kupoteza fahamu.

Chanzo cha tukio hilo kimedaiwa kuwa tabia na wenzake walimuita Salome na kumtuhumu kuwatangazia kwa watu wanachepuka ndoa zao.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki (katikati), akimpa kikombe cha uji wa ulezi, mtafiti wa zao la ulezi Dk. Denis Tippe, wakati wa zoezi la uhamasishaji wa unywaji wa uji huo, kituoni hapo, jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Miundombinu bora yapunguza gharama usafirishaji

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

WAKULIMA wa tumbaku, Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, wamesema uboreshaji wa miundombinu ya barabara wilayani humo, umeanza kupunguza gharama za uzalishaji wa zao hilo na sasa gharama za usafirishaji wa pembejeo zimepungua.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wakulima wa maeneo ya Mtande na Matwiga, walisema awali wakati barabara hazijaboreshwa walikuwa wanachelewa kupata pembejeo hasa mbolea na kwamba hata wakipata walikuwa wanauziwa kwa gharama kubwa. Mmoja wa wakulima hao, Josephat Hamza, ambaye ni mkulima na mwanachama wa Chama cha Wakulima wa Tumbaku cha Mtande, alisema barabara ya kutoka Mbeya kwenda mpaka Makongorosi imeboreshwa.

Alisema zamani walikuwa wanachukulia mbolea Mbeya Mjini, lakini sasa wanapelekewa mpaka katika maeneo ya vijiji vyao kupitia vyama vya ushirika.

"Tulikuwa tunanunua mfuko mmoja kwa zaidi ya Sh. 80,000, lakini kwa sasa tunanunua kwa Sh. 48,000 na kwa sasa ni rahisi kwa sababu tunanunua kwa jumla," alisema Hamza.

Alikishukuru Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa zao hilo (CHUKTU), kwa kuwadhamini wakulima hao mikopo ya mbolea na pembejeo zingine za zao hilo.

Naye Hamis Juma, ambaye ni mkulima na mkazi wa Kata ya Lualaje, alisema mwaka huu zao hilo halijawafaidisha kutokana na hali ya hewa kuwa mbaya hasa mvua kunyesha zaidi ya kiwango kinachostahili.

Alisema mvua hiyo ilikuwa inasababisha mbolea kutofanya kazi na hata wakati wa kuanika jua lilikuwa halitoshi na hivyo baadhi ya mazao yao kuharibika kwa kuwa na rangi ambazo hazitakiwi.

"Tunashukuru sasa hivi tunapata mbolea kwa bei ndogo, lakini naamini tutanufaika zaidi mwakani, mwaka huu tulipata fedha ambazo zilitusaidia tu kulipa madeni," alisema Juma.

Aliiomba serikali kuwasaidia kupata wanunuzi wapya wa zao hilo ili kuongeza ushindani wa bei kwa kuwa sasa kuna mnunuzi mmoja pekee.



# Rais Shein aisifu miongozo, ilani CCM

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, amesema juhudi za serikali za kuwahamasisha na kushirikiana na wananchi na asasi mbalimbali kudumisha amani, ni utekelezaji wa miongozo ya Ilani ya CCM ya uchaguzi ya mwaka 2015-2020 na ya 2020-2025.

Dk. Shein alisema hayo katika uzinduzi wa kongamano la amani kitaifa, lililofanyika Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuhubiri umoja na mshikamano na kupinga ubaguzi wa aina zote.

Alinukuu vifungu vya Ilani ya 2015-2020 (Ibara ya 127), kinachobainisha dhamira ya kuendeleza sera ya kuwaunganisha wananchi wa Zanzibar katika kipindi cha 2015 -2020 CCM pamoja na kuendelea kuwa muumini wa kweli wa amani na utulivu, ili kuimarisha mafanikio yaliokwisha kupatikana.

Alisema chama hicho kimeielekeza serikali kuendeleza jitihada za kuihamasisha jamii umuhimu wa amani, umoja na mshikamano ili kujenga mazingira ya kuaminiana, kuvumiliana na kushirikiana katika masuala mbalimbali ya kijamii.

Kadhalika, kimeielekeza serikali kuendelea kupiga vita na kudhibiti vitendo vya ubaguzi vinavyojitokeza katika sehemu za utoaji huduma za kiuchumi, kisiasa na kijamii miongoni mwa wananchi.

Dk. Shein alisema kongamano hilo ni muhimu kwa wananchi wa Zanzibar kwa kuzingatia kuwa maudhui yake makuu yanahusiana na wajibu wa serikali wa kulinda amani na usalama kama ilivyoelezwa ndani ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Alisema Katiba ya Zanzibar ya 1984 kifungu cha 9 (1) na (2) b na c, kimebainisha Zanzibar itakuwa nchi ya kidemokrasia, usalama na hali nzuri kwa wananchi itakuwa ndiyo lengo kubwa la serikali pamoja na kuhakikisha wananchi washiriki katika serikali yao.

Pia, katika kipindi cha uchaguzi, nchi nyingi duniani hukumbwa na majaribio yenye kuashiria uvunjifu wa amani, baadhi yake hushindwa kudhibiti matokeo hayo na kupata athari mbali mbali, ikiwamo ya kiuchumi.

Dk. Shein, alisema athari nyingine zinazopatikana kutokana na uvunjifu wa amani ni baadhi ya vyama vya siasa kufanya kampeni zenye kuwagawa watu kwa misingi ya dini zao, makabila, uwezo au sehemu wanazotoka.

Naye Makamu wa Pili wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd, aliwataka Wazanzibari na Watanzana kuienzi amani kwa kutambua kuwa kuna watu wengi wanaolionea wivu taifa kutokana na tunu hiyo adhimu.

Aliwataka viongozi wa dini zote nchini na wadau wengine kuungana na kupambana na wote wenye nia ya kutaka kuvuruga amani.

Mgombea urais wa Zanzibar kupitia CCM, Dk. Hussein Mwinyi, alisema wakati huu vyama vya siasa vikinadi sera zao kuelekea uchaguzi mkuu, ni vyema kusisitiza uwapo amani nchini, kwa kuwa hakuna maendeleo yoyote yatakayopatikana bila amani.

Mgombea wa urais kupitia Chama cha ADC, Hamad Rashid Mohamed, alisema nchi nyingi za kiafrika zimeingia katika migogoro na uvunjifu wa amani kutokana na uchu wa madaraka wa baadhi ya viongozi wake pamoja na kugombea rasilimali za taifa.

Kwa upande wake mgombea wa urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ADA-TADEA, Juma Ali Khatibu, aliwataka Wazanzibari kuithamini amani kama mboni za macho yao, kabla na hata baada ya uchaguzi mkuu, na kukemea kauli za wanasiasa wanaohamasisha uvunjifu wa amani kwenye majukwaa.



Mratibu wa wanawake na watoto kutoka shehia ya Kiembe Samaki, Mwanakheri Iddi, akizungumza katika mkutano wa wadau wa malezi, ulinzi na usalama wa mtoto, ulioandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) na SOS, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZEC: Tunathamini watu wenye ulemavu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji Hamid Mahoud, amesema Tume inathamini michango ya watu wenye ulemavu kwa kuwa nao ni wadau wa uchaguzi.

Alisema katika kuthamini michago yao, Tume hiyo imeanzisha vitambulisho maalumu kwa watu wenye ulemavu ili kuwarahisishia kupiga kura bila ya usumbufu.

Aliyasema hayo wakati akifungua semina kwa watu wenye ulemavu wa usikivu (viziwi), mjini hapa.

Alisema pia Tume imejipanga kuweka wakalimani wa alama katika vituo vyote vya kupigia kura, ili kuondoa changamoto kwa watu hao.

Akitoa mada, Mkurugenzi wa Uchaguzi, Thabit Idarusi Faina, alisema jumla ya watu wenye ulemavu wa usikivu 1,268 wameandikishwa katika daftari la kupigia kura na wanatarajiwa kupewa vitambulisho maalum ili iwe rahisi kupiga kura.

"Tuwaambie ndugu zetu wenye ulemavu msiwe na wasiwasi tumewaandalia mazingira mazuri siku ya uchaguzi, ili muweze kupiga kura bila ya usumbufu," alisema Faina.

Washiriki wa semina hiyo walisema wanafarijika zaidi kuona Tume hiyo inavyo wajali watu wenye mahitaji malum kuwashirikisha katika kupata haki zao za msingi.

# Dk. Mwinyi aahidi kuboresha huduma za afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia CCM, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema akichaguliwa kuwa rais atajenga hospitali ya wilaya katika Wilaya ya Kaskazini B Unguja na kujenga nyumba za wahudumu wa afya.

Pia, ataongeza bajeti ya afya, kununua vifaa tiba na kuongeza ajira kwa wahudumu wa afya, ili kutoa huduma bora na kuondoa tatizo la wananchi kufuata huduma hiyo wilaya zingine.

Aliyasema hayo wakati akiwahutubia wananchi na wafuasi wa chama hicho Kijiji cha Bubwini, wanakotokea wazazi wake.

Alisema atahakikisha anajenga barabara kutoka Mahonda hadi Bubwini, ili kuondoa mzunguko kwa wananchi kutoka wilaya moja kwenda nyingine.

"Nitajenga daraja katika Mto wa Zingwezingwe kwa kuwa Bubwini kutakuwa na bandari ya kisasa, lazima kuwe na daraja kuwawezesha wananchi kupita."

Alisema ujenzi wa miundombinu hiyo utaimarisha uchumi kwa wananchi wa wilaya hiyo.

Pia, Dk. Mwinyi aliahidi kujenga shule ya ghorofa ya sekondari na bweni la wanafunzi katika kijiji cha Gongoni Bubwini, ili kupunguza msongamano wa wanafunzi shuleni.

Alisema ataifanyia kazi changamoto ya wizi wa mifugo na kwamba atahakikisha anajenga kiwanda cha maziwa ili wafugaji wanufaike na sekta hiyo.

"Lazima tukomeshe wizi wa mifugo ili wafugaji wanufaika na mifugo kwa kuzalisha maziwa kwa wingi na kupeleka viwandani," alisema.

Alisema wilaya hiyo imepata bahati ya kujengwa bandari kubwa ambayo itakuwa kitovu cha kutoa ajira kwa wingi visiwani humo.

Dk. Mwinyi alisema bandari hiyo haitoathiri shughuli za kijamii za wananchi kama uvuvi, kilimo cha mwani na uanikaji wa dagaa.

Alisema pia atawawezesha wananchi kiuchumi hasa wanyonge wakiwamo wajasiriamali kwa kupatiwa mafunzo na nyenzo muhimu.

Pia, ataimarisha huduma ya majisafi na salama katika wilaya hiyo na nyingine zenye changamoto hiyo, ili wananchi wapate huduma hiyo muhimu.

Dk. Mwinyi aliahidi kuifanya Zanzibar ya viwanda ili kuwa na soko la uhakika wa bidhaa mbalimbali ikiwamo maziwa na samaki na vijana kupata ajira.

Kadhalika, ataimarisha sekta ya utalii ambayo inazalisha pato kubwa la taifa na utalii kunufaisha wananchi wa maeneo husika.

Aliwataka wawekezaji wa sekta hiyo kuchangia maendeleo ya wananchi katika maeneo waliyowekeza na kununua kila kinachotegenezwa nchini badala ya kuagiza kutoka nje ya nchi.

Atazuia athari zitokanazo na utalii ikiwamo suala la dawa za kulevya na mporomoko wa maadili kwa wananchi.

Aliahidi kufafanya kazi na wananchi ili kupiga hatua katika maendeleo.

Naye Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, alisema kuwa Dk. Mwinyi ni mtu hodari na mchapa kazi hivyo wananchi wakimchagua atawaletea maendeleo.

"Imani yangu kwamba yale yote niliyoyafanya, Dk. Mwinyi atayaendeleza na kuyamaliza na yale ambayo sijayamaliza atayamaliza ili kuwaleteeni maendeleo," alisema Dk. Shein.

# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EMMY MICHAEL MWEPA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **Toyota IST** yenye namba za usajili **T 388 DLK.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi **MBE/MBE/RB/723953/2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ARNOLD FRANCIS JOSEPH**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA LAND CRUISER PRADO** yenye namba za usajili **T 800 ACB**
Chassis No. **LJ780008502**
Engine **No. 2L2498548**
Yenye rangi GRAY
Yeyote atakayeiona atoe taarifa Polisi.
Taarifa ya Polisi:
**MWA/NY/RB/285836/2020**

115936902

**IN THE DISTRICT COURT OF ILALA AT SAMORA AVENUE**

**CIVIL CASE CAUSE NO. 27...2020**

**ZENICE B. MBOYA.............PLAINTIFF/APPELEANT**

**VERSUS**

**WALTER PHILIPO SHAYO & 1...........................DEFENDANT/RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE MENTION/HEARING**

**The NOTICE** that the above case has been fixed for Mention/Hearing on 21 day of 10....2020 at 8:30 a.m before Hon. KANJE RM. YOU ARE required to appear in this Court without fail and you must produce to that day all the document upon which you intended to reply in support of your case. Given under my hand and seal of the court this **28 day of 9...2020**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

MIRATHI Na. 51 YA MWAKA 2020
**MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI**
Ombi la **NIMESHI RASHMI**
Taarifa ya kawaida **( KANUNI YA 75)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa apo juu wanafahamishwa kufika nakuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/ mwombaji apo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe **21 mwezi wa Oktoba 2020.**

215936202

## TANGAZO

**SOUTHERN HIGHLANDS AGRICULTURAL DEVELOPMENT COMPANY LIMITED**

**Registration No. 64588**
Bodi ya wakurugugenzi kwa pamoja na wamiliki wakampuni ya **SOUTHERN HIGHLANDS AGRICULTURAL DEVELOPMENT COMPANY LIMITED** wameamua kufunga kampuni yao baada ya kuendeshwa kwa hasara. Bodi hiyo pia imemchangua bwana **ENOCK A. NDONDOLE** kuwa msimamizi wa zoezi la ufungaji wa kampuni hiyo. Kwa yeyote mwenye madai na kampuni hii awasiliane na bwana **ENOCK A. NDONDOLE.**

115937502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IRENE BRUCE KASAMBALA**
anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya
**TOYOTA VOLTZ**
yenye namba ya usajili
**T402 DEF.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kwenye kituo chochote cha Polisi.
Taarifa ya Polisi namba
**WMB/RB/420/2020.**

215936102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;302/2020**

**Ombi la REDEMPTA BLANCE URASSA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu DAVID GABRIEL MAKALA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 05/10/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 08/10/2020.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU

115936702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11 (S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya MAKOLE**

**Usimamizi wa Mirathi No. 96/2020.**

**Ombi la ROMAN FIDY ROMAN kuteuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu FIDY ROMAN GOSA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri wakitaka mnamo tarehe 22/10/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo. Tarehe07/10/2020.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MAKOLE
DODOMA

115936502


Uza,
Chenye Thamani
Kubwa Kwa Kutangaza
Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Nzi auteka mdahalo urais Marekani

**WASHINGTON, Marekani**

WAKATI mdahalo wa makamu wa urais umenoga, tukio la nzi kutua kichwani kwa mgombea mmojawapo aliuteka mweleko wa mjadala hata kufikia hatua ya baadhi kubatizana majina papo kwa hapo.

Hiyo ilikuwa baada ya nzi kutua na kukaa kwa takriban dakika mbili kichwani kwa Makamu wa Rais, Mike Pence na ghafla akauteka umaarufu wa kikao

Kama ilivyo kawaida ya matukio hayo kufuatiliwa kwa karibu mitandao jamii, kwenye mtandao wa Twitter tukio lilijadiliwa zaidi ya mara 700,000 tangu kushuhudiwa wakati mdahalo unaendelea.

Licha ya wagombea hao kujitahidi kwa kila namna kwenye hoja zao, hakuna walichosema kilichoendana na watu waliokuwa wanawafuatilia kupitia mitandaoni kama ilivyokuwa kwa nzi aliyejitokeza ambaye hakutarajiwa.

Kampeni ya Joe Biden nayo imetumia vizuri fursa hiyo kwa kusambaza maneno "flywillvote.com".

Nzi huyo ameunganisha pande zote mbili huku mmoja akimpachika jina la shujaa wa Marekani na mwingine akisema huenda ndio jambo litakalokumbukwa zaidi.

Aidha, mmoja amelinganisha wakati wa mdahalo wa urais katika uchaguzi uliotanguliwa miaka minne iliyopita ambapo nzi alijitokeza juu ya kichwa cha mgombea urais Hillary Clinton.

Hilo halimaanishi kwamba nzi huyo ni yule yule aliyejitokeza wakati huo na sasa amerejea tena.

Lakini siyo wote waliomchukulia nzi huyo kwa utani kwa sababu mchambuzi mwenye msimamo mkali, Ben Shapiro kusema kuwa nzi huyo ni njia moja ya kutatiza kile kilichokuwa kinaendelea wakati wa mdahalo.

*BBC*



Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta (kushoto) na Rais wa Misri, Abdel Fattah al-Sisi (kulia) wakutana kujadili mzozo wa mto Nile. **PICHA: IKULU KENYA.**

# Maambukizi corona yapanda Ujerumani

**BERLIN, Ujerumani**

WAZIRI wa Afya wa Ujerumani, Jens Spahn, amesema nchi hiyo inapita katika kipindi kinachotia hofu baada ya kesi za maambukizi ya virusi vya corona kupanda.

Maambukizi mapya ya kila siku yameongezeka na kupita 4,000 tangu Aprili.

Mkuu wa Taasisi ya Udhibiti wa Magonjwa ya Robert Koch, Lothar Wieler, ameonya kwamba Ujerumani inaweza kushuhudia usambaaji wa corona ambao hautaweza kudhibitiwa.

Kwa mujibu wa taasisi hiyo, nchi hiyo yenye uchumi mkubwa barani Ulaya ilirekodi maambukizi mapya ya corona 4,058 katika muda wa masaa 24, ikiwa ni ongezeko kubwa katika idadi iliyotolewa juzi ya watu 2,828,

"Takwimu hizo zinaonyesha ongezeko linalotia hofu," Waziri wa Afya wa Ujerumani, Jens Spahn aliwaeleza waandishi wa habari mjini Berlin.

Waziri huyo aliwataka Wajerumani kutopuuzia hatua za kuzuwia usambaaji wa virusi hivyo hatari.

"Hakuna nchi nyingi barani Ulaya ambazo zimeweza kupambana na tatizo hili. Lakini hatuwezi kuchukulia kama mchezo wa kamari kile ambacho tumefanikiwa hadi sasa," alisema Spahn.

Majimbo 16 ya Ujerumani yameimarisha sheria kwa ajili ya safari za ndani, ambapo wengi wakikubaliana na marufuku ya kukaa katika hoteli au nyumba za kupanga wakati wa likizo kwa wasafiri kutoka katika maeneo yanayofahamika kama yenye hatari nchini humo.

Serikali ya Uingereza inatafakari kuweka vizuwizi vipya katika maisha ya kila siku huku kukiwa na ushahidi kuwa hatua hadi sasa hazijaleta mafanikio ya kutosha kuzuwia maambukizi mapya ya corona.

Wakati idadi ya watu wanaohitaji kwenda hospitali wakiwa na dalili zinazoelekea kuwa na maambukizi ya corona ikiongezeka, na katika baadhi ya maeneo Kaskazini mwa Uingereza hali ikiwa ni mbaya, shinikizo dhidi ya serikali kuchukua hatua zaidi linaongezeka.

Kampuni ya Gilead Sciences ilisema jana kuwa imekubali kuizuia Ulaya hadi dozi 500,000 la dawa ya remdesivir, wakati bara hilo linahangaika kuongeza upatikanaji wake ambayo ni moja kati ya dawa aina mbili zilizothibitishwa hadi sasa kutibu wagonjwa wa corona. Makubaliano hayo yanajumuisha ununuzi wa dawa hiyo kwa miezi sita ijayo kwa mataifa 27 wanachama wa Umoja wa Ulaya (AU), Uingereza, mataifa sita ya eneo la balkan pamoja na Iceland, Liechtenstein na Norway.

*DW*

# Waziri Mkuu wa zamani Mali aachiwa

**BAMAKO, Mali**

MALI imemuachilia Waziri Mkuu wa zamani, Boubou Cissé, aliyekuwa amekamatwa.

Mamlaka ya nchi hiyo imetangaza kuachiliwa huru kwa wanasiasa kadhaa na wanajeshi waliokamatwa wakati wa mapinduzi ya Agosti.

Walioachiliwa ni pamoja na aliyekuwa Waziri Mkuu, Cissé.

Taarifa rasmi imeonyesha kwamba waliokamatwa bado watasubiri uamuzi wa mahakama ikiwa kutakuwa na haja ya kufanya hivyo.

Jumatatu, serikali ya mpito ilitangaza baraza jipya la mawaziri ambapo wanajeshi waliopanga mapinduzi walikabidhiwa nafasi muhimu serikalini ikiwemo ulinzi, usalama, utawala wa mipaka na maridhiano ya kitaifa.

Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS), imeiondolea Mali vikwazo na kutambua kile ilichokitaja kama kupigwa kwa hatua muhimu kuelekea kwenye utaratibu wa kikatiba.

BBC

# WB yatabiri uchumi wa Afrika kuimarika 2021

**WASHINGTON, Marekani**

BENKI ya Dunia (WB), imesema janga la virusi vya corona limeathiri ukuaji wa uchumi barani Afrika na huenda ukashuka kwa asilimia 3.3 mwaka huu.

Haya hivyo, benki hiyo inatabiri kuimarika kwa uchumi huo mwaka 2021.

Hadi kufikia sasa, Afrika imefanikiwa kukwepa athari kubwa za janga la corona huku idadi ya maambukizi ikiwa chini ikilinganishwa na mabara mengine.

Lakini, hatua ya kutotoka nje ili kukabiliana na janga hilo imesababisha ukuaji wa kasi ya chini ya uchumi, hususani Afrika Kusini ambayo ni nchi ya pili yenye ukuaji mkubwa wa uchumi.

Benki wa Dunia imeonya kwamba raia zaidi ya milioni 40 huenda wakatumbukia kwenye umaskini.

*BBC*

**Hadi kufikia sasa, Afrika imefanikiwa kukwepa athari kubwa za janga la corona huku idadi ya maambukizi ikiwa chini ikilinganishwa na mabara mengine.**




Mgombea Urais kupitia Chama cha Wananchii (CUF), Ibrahim Lipumba akihutubia mkutano wa kampeni, jijini Arusha juzi.
**PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Kada wa CHADEMA afanyiwa unyama

**Na Allan Isack,**

KADA wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Evarist Rite, mkazi wa Narumu, Hai mkoani Kilimanjaro, ameokotwa akiwa amejeruhiwa vibaya na watu wasiojulikana.

Mtu huyo aliokotwa jana akiwa ametelekezwa kando ya barabara kuu ya Arusha-Moshi, mji mdogo wa Kikatiti, Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha.

Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Arusha, Elias Mungure, alisema majira ya saa 11:00 jioni ya juzi, alipigiwa simu na wananchi na baadhi ya makada wa chama hicho wakimweleza kuwa kuna kada wa chama wamemkuta ametupwa barabarani.

"Tuliondoka vijana wetu kwenda eneo la tukio na tulipofika, tulimkuta Evarest akiwa ametupwa barabarani, anavuja damu kwenye ulimi, mikono, vidole, sehemu za siri na amevunjwa meno mawili ya mbele," alisema Mungure.

Kwa mujibu wa Mungure, mtu huyo alitupwa karibu na kituo cha mafuta na kwamba waliofichua taarifa hizo ni pamoja na wafanyakazi wa kituo hicho, ambao walipiga simu Kituo cha Polisi na askari kufika eneo la tukio na kumhoji kada huyo.

"Kutoka kituo cha mafuta hadi kituo cha polisi kuna umbali wa mita 100 na baada ya hapo tulisafiri hadi Wilaya ya Hai, tulichukua PF3 (fomu ya polisi namba tatu) kwa ajili ya matibabu.

"Baada ya kuchukua fomu hiyo, tulimpeleka Hospitali ya Wilaya ya Hai kwa ajili ya kupatiwa matibabu. Tuliwasiliana na viongozi wetu wa chama Wilaya ya Hai.

"Walipofika hospitalini hapo, walithibitisha kumfahamu kada huyo na walisema kuwa walikuwa wamempangia majukumu ya kwenda kuchukua mabango ya chama," alisema.

Mungure alisema walipofika eneo la tukio walimkuta kada huyo akiwa anatokwa na damu sehemu mbalimbali za mwili.

Alipotafutwa kuzungumzia tukio hilo, Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi (ACP) Salum Hamduni, alisema bado hajapokea taarifa zozote kuhusiana na tukio hilo.

# Magufuli kunguruma Dar leo

**Na Gwamaka Alipipi**

MGOMBEA urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, leo anaendelea kufanya kampeni katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu chama hicho, ikiwamo mwendelezo wa kampeni.

Polepole alisema Dk. Magufuli baada ya kumaliza shughuli za kiserikali, ataendelea kufanya kampeni kwa siku nne jijini Dar es Salaam, baadaye kuendelea katika mikoa mingine.

"Kesho (leo) Dar es Salaam inakwenda kusimama. CCM inakwenda kuandika historia. Mgombea urais Dk. John Magufuli anakwenda kufanya mkutano mkubwa ambao haujawahi kutokea," alisema.

Aliongeza kuwa Dk. Magufuli atatumia mkutano huo kuelezea mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano kwenye jiji la Dar es Salaam, pamoja na mikakati ijayo ambayo imeainishwa katika Ilani.

Alisema Jiji la Dar es Salaam kwa sasa liko tofauti na miaka iliyopita kutokana na kujengwa kwa miundombinu ya kisasa ikiwamo barabara, madaraja, barabara za juu pamoja na huduma za kijamii.

Pia alisema mgombea urais wa CCM visiwani Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, naye anaendelea vizuri na kampeni na kwamba atashinda kwa kishindo kikubwa huku mgombea mwenza wa urais, Samia Suluhu Hassan, akiendelea na kampeni na sasa yuko Mpanda mkoani katavi.

"Kwa ujumla tupo vizuri, endapo uchaguzi ungefanyika sasa Dk. Magufuli angeibuka na ushindi wa zaidi ya asilimia 90, wabunge asilimia 75 na madiwani asilimia 80," alisema Polepole.

Kuhusu baadhi ya watu wanaobeza maendeleo yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano, Polepole alisema: "Unapotaka kuleta maendeleo ya watu ni lazima ulete na maendeleo ya vitu, tumejenga shule za sekondari na msingi na wanaosoma ni watu.

Aliongeza: "Tumejenga madaraja, fly over, hayo yote ni maendeleo ya vitu lakini wanaoteleza juu ya hayo madaraja ni watu. Maendeleo ya vitu yanakwenda sambamba na maendeleo ya watu."

# Ajali yakatisha maisha ya hakimu

**Na Romana Mallya**

WATU wawili, akiwamo Hakimu Zakoleo Sanga (42) mkazi wa Chunya mkoani Mbeya, wamefariki dunia baada ya gari dogo walilokuwa wakisafiria kuligonga lori.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Kamishna Msaidizi (ACP) Juma Bwire, alisema ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa tatu usiku wilayani Mufindi na kumjeruhi mtu mmoja.

Alimtaja mtu mwingine aliyefariki dunia kwenye ajali hiyo iliyotokea eneo la Changarawe kuwa ni dereva David Guriko.

Alisema ajali hiyo ilihusisha gari lenye namba za usajili T 331 DSJ aina ya Toyota Brevis ambalo liligonga lori lenye namba T 575 ABS aina ya Benz.

Kamanda Bwire alisema katika ajali hiyo, abiria mwingine aliyekuwa kwenye Brevis, Samuel Richard (34) mkazi wa Iringa, alijeruhiwa na amelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mufindi, mjini Mafinga.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi wa gari dogo aina ya Brevis ambalo liliingia chini ya lori.



# HISPANIA, URENO
## WENYEJI KOMBE LA DUNIA LA 2030

**NYON, Uswisi**

HISPANIA na Ureno zimethibitisha kuomba kuandaa kwa pamoja michuano ya Kombe la Dunia ya mwaka 2030.

Nchi mbili hizo zilitangaza Desemba kwamba zitachunguza namna ya kuandaa michuano hiyo ya soka mikubwa zaidi duniani, wakiiondoa Morocco - ambayo awali ilitajwa kuhusika nao na kuwa nchi ya tatu.

Kabla ya mchezo wa kirafiki wa Jumatatu kati ya nchi hizo mbili uliomalizika kwa sare mjini Lisbon, Jumatano, mashirikisho ya soka ya Hispania na Ureno yalithibitisha makubaliano hayo.

"Makubaliano haya yana maana kubwa katika hatua ya kufanikisha jambo hili, lakini ni muhimu kwa nchini zenyewe," alisema Rais wa Shirikisho la Soka la Hispania (RFEF), Luis Rubiales katika taarifa yake.

"Soka ni mchezo wenye ushawishi mkubwa na kwa hakika tunataka kuhakikisha jambo hili linafanikiwa kwa umakini mkubwa."

"Vitu vichache vinaweza kuwa vya kuvutia zaidi na tunafikiri tutakuwa na upatina mzuri zaidi na Ureno. Tutakwenda mkono kwa mkono na Shirikisho la Soka la Ureno."

Qatar ndio mwandaaji wa michuano ijayo ya mwaka 2022, huku Canada, Marekani na Mexico wataandaa fainali zitakazofuata za mwaka 2026.

# WIJNALDUM: BARCELONA HAIKUWA NA NIA NA MIMI

**LIVERPOOL, England**

KIUNGO wa Liverpool, Georginio Wijnaldum amesema hafikirii kama Barcelona ilikuwa na dhamira ya dhati ya kumtaka ahamie pale Camp Nou.

Kiungo huyo raia wa Uholanzi alikuwa anahusishwa kujiunga na miamba ya soka la Ulaya, Barcelona baada ya timu hiyo kuchukuliwa na kocha, Ronald Koeman.

Mkataba wa Wijnaldum unamalizika mwishoni mwa msimu ujao wa Ligi Kuu England.

"Ilivyokuwa, ilionekana wazi kuwa ningebakia Liverpool," alisema kiungo huyo mwenye umri wa miaka 29 akinukuliwa na Dail Mail.

"Mkataba wangu umebakiza kama miezi 10, hivyo kila jambo linawezekana, hauwezi kujua katika soka nini kitatokea."

Juu ya matamanio ya Barcelona juu yake, Wijnaldum amesema hafikirii kama walikuwa na nia ya dhati kiasi hicho.

Liverpool ilimsajili Wijnaldum akitokea Newcastle United mwaka 2016 kwa ada ya uhamisho wa pauni milioni 25.




Ameisaidia timu hiyo kushinda taji la EPL, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la Dunia ngazi ya klabu.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp awali mwanzoni mwa msimu huu alisema mahusiano yake na mchezaji huyo yanaendelea vizuri.

# BEKI INTER MILAN AKUTWA NA CORONA

**MILAN, Italia**

BEKI wa Inter Milan, Milan Skriniar, amekutwa na virusi vya ugongwa wa corona wakati timu yake ya Taifa ikiwa katika mchezo muhimu wa hatua ya mtoano ya nusu fainali ya Kombe la Euro 2020 dhidi ya Jamhuri ya Ireland.

Nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Slovakia alibainika kuwa na ugonjwa huo baada ya kurejea nchini kujiandaa na mchezo huo ulioko kwenye kalenda ya kimataifa ya FIFA.

Tayari timu yake ilikuwa imeshajiandaa kumkosa kiungo, Stanislav Lobotka, ambaye naye amelazimika kukaa karantini na wachezaji wenzake wa klabu ya Napoli.

Mchezaji wenzake na Skriniar wa Inter Milan, Alessandro Bastoni naye amekuwa na corona na hivyo wamelazimika kujitenga ili kupunguza kasi ya maambukizi ya ugonjwa huo kwenye Serie A.

Wiki iliyopita kikosi cha Juventus kililazimika kuanza kujiweka karantini baada ya wachezaji wake wawili (majina hayakuwekwa wazi) kukutwa na virusi vya ugonjwa huo.

Kwa hali hiyo, Ireland inapewa nafasi kubwa ya kuibuka na ushindi katika mechi hiyo kutokana na nyota wawili bora wa Slovakia, Lobotka na Skriniar kuukosa mchezo huo. Pia golikipa wao Martin Dubravka huenda akaukosa mchezo huo kwa sababu ya majeruhi.

Skriniar pia alikuwa katika mawindo na klabu inayoshiriki Ligi Kuu England kwenye dirisha hili la usajili na mwezi uliopita, Tottenham ilifanya mazungumzo na Inter Milan kuhusiana na uhamisho wa nyota huyo.

Hata hivyo, mazungumzo ya klabu hizo mbili yalikuwa mbali kwa sababu ya dau ambalo Wataliano hao wanataka kulipwa la pauni milioni 52, ili kumuuza beki huyo wa kati na kiasi ambacho Spurs iko tayari kulipa.

Fulham pia ilitajwa kuwa kwenye mbio za kuwania saini ya beki huyo, lakini klabu hiyo ilishindwa kukamilisha mchakato huo na kuamua kuachana naye.





# CAVANI

## KUIKOSA NEWCASTLE, PSG

**MANCHESTER, England**

NYOTA mpya wa Manchester United, Edinson Cavani ambaye amesajiliwa katika siku ya mwisho ya dirisha la usajili, atachelewa kuanza kuitumikia timu hiyo baada kuonyesha dalili za maambukizi ya corona.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, Cavani atatakiwa kujitenga mwenyewe kwa siku angalau 14 kwa matazamio zaidi.

Nyota huyo raia wa Uruguy alijiunga na United Jumatatu iliyopita kwa uhamisho huru baada ya kumaliza mkataba wake kule PSG, Juni mwaka huu.

Mchezo ujao wa United utakuwa dhidi ya Newcastle United utakaopigwa Oktoba 17, mwaka huu katika dimba la St James Park.

Bila shaka itakuwa maumivu kwa kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer, ambaye atakuwa bila strika wake raia wa Ufaransa, Anthony Martial ambaye alionyeshwa kadi nyekundu.

Cavani ameshindwa kujiunga na wachezaji wake wapya hadi hapo hali itakapotengamaa na kuna uwezekano pia akakosa mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Paris St-Germain, mchezo wa ugenini utakaochezwa Oktoba 20, mwaka huu.



## DE BOER AFUNGUKA KUHUSIANA NA KICHAPO

**AMSTERDAM, Uholanzi**

FRANK de Boer amesisitiza mara zote alitaka kushinda baada ya kufungwa 1-0 na Mexico kwenye mchezo wake wa kwanza kama kocha mkuu wa Uholanzi.

Lakini amesisitiza kwamba hiyo sio mara ya kwanza kwa kocha kufungwa kwenye mechi yake ya kwanza.

Raul Jimenez alifunga kipindi cha pili kwa penalti katika mchezo huo wa kirafiki uliopigwa dimba la Johan Cruijff Arena, juzi Jumatano, ambapo ilishuhudia De Boer akicheza dhidi ya kocha wa Mexico, Gerardo Martino - ambaye alimrithi kuchukua mikoba yake kule kwenye Ligi Kuu ya Marekani, MLS, Atlanta United.

De Boer aliondoka Atlanta Julai, mwaka huu baada ya matokeo mabaya na akateuliwa kuchukua nafasi ya Ronald Koeman kuwa kocha wa Uholanzi.

Inter Milan walimfukuza De Boer baada ya kuiongoza timu hiyo kwa siku 85 mwaka 2016, na mlinzi huyo wa zamani wa Uholanzi, aliiongoza Crystal Palace kwenye mechi saba tu kama kocha wake mwaka uliofuata kabla ya kutimuliwa.

Katika mchezo wake huo wa kwanza wa kimataifa, aliwachezesha kwa mara ya kwanza, Owen Wijndal na Teun Koopmeiners, huku akiwapumzisha wachezaji wenye majina makubwa kama Frenkie de Jong na Daley Blind kwa ajili ya mchezo wa Jumapili wa Ligi ya Mataifa ya Uefa dhidi ya Bosnia-Herzegovina na Italia siku tatu baadaye.

"Bila shaka nina hisia mbaya," alisema De Boer akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo. "Mara zote nilitaka kushinda. Lakini tulifanya machaguo kadhaa, kitu ambacho nafikiri niliumia sana tu."

## LOW AKERWA SARE YA TATU UJERUMANI

**COLOGNE, Ujerumani**



KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Joachim Low amesema hakuridhishwa na kikosi chake kusalimu amri na kukubali sare ya 3-3 baada ya kuongoza mara tatu dhidi ya Uturuki.

Kenan Karaman alifunga dakika ya mwisho mwenye mchezo huo wa Jumatano wa kirafiki kufuta bao la Gian-Luca Waldschmidt la dakika ya 81 na sasa Ujerumani haijashinda mechi tatu kwa mwaka 2020.

Julian Draxler na Florian Neuhaus aliyekuwa anacheza kwa mara ya kwanza, pia waliiweka mbele Ujerumani mapema kwenye mchezo huo, huku Ozan Tufan na Efecan Karaca nao wakisawazisha.

Ujerumani pia ilisalimu amri baada ya kuongoza kwa bao moja na kutoka sare ya 1-1 na Hispania na Uswisi mwezi uliopita, na Low alikubali kwamba kikosi chake kinatakiwa kufanyiwa kazi.

"Tatizo sasa limekuwa na muda mrefu," alisema baada ya mchezo huo akiwaambia waandishi wa habari.

"Timu haijawahi kucheza kwa pamoja kama hivi, siwezi kuwalaumu sana.

"Hilo linatokea kwa wachezaji wengine pia. Lakini nimekatishwa tamaa na kiwango cha timu kinavyocheza kwa sasa."

Ujerumani ilifanya mabadiliko saba kutoka kwenye kikosi chake cha hivi karibuni.

Hata hivyo, Low hakuwa anatafuta sababu ya kujitetea bada ya sare hiyo ya tatu hapa Cologne, ambapo wachezaji 300 waliruhusiwa kuhudhuria.

"Kuchoka haiwezi kuwa sababu, sio sababu ya kujitetea au kuelezea," alisema.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GIROUD AKARIBIA REKODI YA HENRY

●●●Afikisha idadi ya mechi 100 katika kikosi cha Ufaransa huku pia akitupia magoli mawili...

**PARIS, Ufaransa**

OLIVIER Giroud anakaribia kuifikia rekodi ya Thierry Henry ya kuwa mfungaji wa wakati wote wa Ufaransa baada ya kufunga mara mbili wakati akicheza mechi yake ya 100 ya kimataifa.

Straika huyo wa Chelsea alifunga bao lake la 41 na 42 kwa Les Bleus hao Jumatano wakati wakiibuka na ushindi wa magoli 7-1 dhidi ya Ukraine kwenye mchezo wa kirafiki pale uliochezwa Stade de France.

Giroud amempita Michel Platini kwenye orodha hiyo na sasa yupo nyuma ya nyota wa zamani wa Arsenal na Barcelona, Henry, ambaye alifunga mabao 51 katika mechi 123.

Giroud amekuwa akitumiwa sana na kocha, Didier Deschamps kama ndiye mfungaji wake, licha ya kuwachezesha mafowadi wengine kama Antoine Griezmann na Kylian Mbappe.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 aliichezea Ufaransa mechi zote saba kwenye Kombe la Dunia mwaka 2018, ikiwamo ile ya fainali ambapo walishinda mabao 4-2 dhidi ya Croatia, ingawa hakufunga bao lolote.

Ingawa hafikirii sana kufikia rekodi ya Henry, lakini amebainisha kwamba rekodi yake hiyo mpya ya kucheza mechi 100 ni kubwa mno kwake.

"Kwa uhakika kabisa, najisikia fahari kubwa," alisema Giroud, ambaye alikuwa nahodha kwenye mchezo huo dhidi ya Ukraine, akiiambia TF1.

"Ni heshima kubwa (kufikisha mechi 100) na nina furaha kubwa imetokea kama hivi.

"Mara zote itakuwa ni ya kuvutia kwangu. Ni mchezo wa kirafiki, lakini nimeweza kufikisha mechi mia moja, hivyo nina furaha kubwa kwa upande wangu pamoja na timu kwa ujumla. Tulionyesha mambo mengi mazuri.

"Sasa naangalia mbele. Natumaini kuendelea kama hivi."

Ufaransa inacheza na Ureno kwenye Ligi ya Mataifa ya UEFA Jumapili.

## KWA UFUPI

**DEMBELE AITAKA JUVE**

MSHAMBULIAJI wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Ousmane Dembele (23), hakuwa na malengo ya kujiunga na Manchester United wakati dirisha la usajili likiwa bado halijafungwa na kueleza mipango yake ni kuhamia Juventus katika majira ya joto mwakani. ***(Catalunya Radio, via Mirror)***

**UNITED YAMKATAA SARR**

MANCHESTER United haitafanya uhamisho wa nyota wa Timu ya Taifa ya Senegal na Watford, Ismaila Sarr (22), kabla ya siku ya mwisho ya kufunga usajili wa EFL ambao ni Oktoba 16, mwaka huu. (Goal)

**ROSE MAMBO MAGUMU**

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho anajiandaa kumwondoa beki wa Timu ya Taifa ya England, Danny Rose (30), kwenye kikosi chake cha wachezaji 25, ambacho kitakamilika ifikapo Oktoba 20, mwaka huu. ***(Mail)***

**OZIL, SOKRATIS WATEMWA**

ARSENAL imewaacha katika kikosi chake, kiungo mchezeshaji wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Mesut Ozil (31) na beki wa kati ya Ugiriki, Sokratis Papastathopoulos (32), kuelekea mchezo wake wa Ligi ya Europa. ***(Talksport)***

**ANDERSON: NDOTO ZIMETIMIA**

NYOTA wa West Ham na Timu ya Taifa ya Brazil, Felipe Anderson amesema "amekamilisha ndoto yake" ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya na klabu yake ya muda mrefu ya Porto, lakini anaamini bado nafasi ndani ya kikosi cha Hammers. ***(Talksport)***

**WEST HAM SOKONI**

WEST Ham bado inahitaji kupata beki mpya wa kati kutoka kwenye michuano ya Championship wakati wakitafuta kiungo wa kurithi mikoba iliyoachwa na Felipe Anderson. ***(London Evening Standard)***

**ROMERO KWENDA MAREKANI**

GOLIKIPA wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Argentina, Sergio Romero (33), anajiandaa kujiunga na Ligi Kuu Marekani baada ya mchakato wake wa kutua Everton kukwama kwenye siku ya mwisho. ***(Mail)***

**KNOCKAERT AWINDWA EPL**

KOCHA mpya wa New Nottingham Forest, Chris Hughton anajiandaa kumsajili kwa mkopo kiungo mshambuliaji wa Fulham Mfaransa, Anthony Knockaert, ambaye ana umri wa miaka 28. ***(Sky Sports)***

**GRANT MAMBO SAFI**

MABOSI wa West Brom wanaamini watakamilisha mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Huddersfield, raia wa England, Karlan Grant (23), kabla ya siku ya mwisho ya kufunga dirisha la usajili la EFL hapo Ijumaa. ***(Mail)***

**RUDIGER KUONDOKA CHELSEA**

KOCHA wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Joachim Low ameweka wazi, Antonio Rudiger "alijaribu kufanya kila njia ili aondoke Chelsea" kabla ya dirisha la usajili halijafungwa, lakini ilishindikana na anaamini beki huyo mwenye umri wa miaka 27 atahakikisha anasaka uhamisho kwenye dirisha la Januari mwakani. ***(Sun)***

**CANTWELL ANUKIA LEEDS**

Norwich inaamini itambakisha kiungo wake, Todd Cantwell ingawa nyota huyo mwenye umri wa miaka 22 anataka kujiunga na Leeds United, inayoshiriki Ligi Kuu England. ***(Football Insider)***

**CAVANI AITAJA BOCA JUNIORS**

MSHAMBULIAJI mpya wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Uruguay, Edinson Cavani (33), amesema atajiandaa kujiunga na Boca Juniors ya Argentina baada ya muda wake wa kuitumikia klabu ya Old Trafford utakapomalizika. ***(Goal)***

# KAULI YA MASAU BWIRE INAVYOWATESA IHEFU FC

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

TIMU ya Ihefu FC kutoka Wilaya ya Mbarali ni moja ya timu tatu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara mwaka huu na kuufanya mkoa wa Mbeya kuwa na timu tatu zinazoshiriki ligi hiyo ya juu nchini.

Ihefu FC ilipanda baada ya kuishusha daraja Mbao FC ya Mwanza kwa kuifunga katika mechi ya mtoano, ikipata ushindi wa mabao 2-0 nyumbani na mchezo wa marudiano uliochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Mbao FC ilishinda magoli 4-2.

Hata hivyo matokeo hayo yaliipa faida Ihefu FC ambayo ilipata nafasi ya kupanda Ligi Kuu kwa faida ya kufunga mabao mawili ugenini na hivyo kuwashusha wabishi Mbao FC. Ihefu ilianza msimu mpya wa Ligi Kuu Bara kwa kufungwa mabao 2-1 na Simba katika mchezo huo uliofanyika Septemba 6, mwaka huu. Shukurani wafungaji, John Bocco na Mzamiru Yasin kwa upande wa mabingwa watetezi huku bao pekee la Ihefu likifungwa na Omary Mponda.

Pamoja na timu hiyo kufungwa lakini iliyonyesha kiwango cha hali ya juu liche ya kuwa ngeni kwenye ligi hiyo ambayo kwa mara ya kwanza inashirikisha timu 18.

Mechi iliyofuata, Ihefu FC ilikuwa mwenyeji wa timu ya Ruvu Shooting FC ya mkoani Pwani, ambapo ilipata ushindi wa bao 1-0 na huo ndio ushindi wa kwanza na wa mwisho kwa timu hiyo katika mechi tano ambazo imecheza kabla ya ligi kusimama kwa muda kupisha maandalizi ya Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Baada ya mchezo huo kumalizika, Msemaji wa Ruvu Shooting, Masau Bwire alitoa kauli ya kuikashifu Ihefu akidai timu hiyo ni mbovu kuliko timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu.

"Tumefungwa na timu mbovu kwenye ligi hii haijawahi kutokea, narudia tumefungwa na timu mbovu haijawahi kutokea, kama hamwamini kwamba Ihefu wabovu subiri mtakuja mniambie," alisema Bwire.

Kauli ya Bwire, ilianza kujidhihirisha kwenye mchezo wa Septemba 18 mwaka huu dhidi ya Mtibwa Sugar, ambapo Ihefu ikiwa mwenyeji iliambulia kipigo cha bao 1-0 na Septemba 27 ilicheza na Mwadui FC na kuambulia kichapo kingine cha mabao 2-0.

Mbali na vipigo hivyo ambavyo Ihefu imeambulia, pia timu hiyo ni miongoni mwa timu zilizopigwa mabao mengi na kufunga machache mpaka sasa ambapo imefunga mabao mawili pekee ambayo iliipata kwenye mechi na Simba pamoja na Ruvu Shooting, lakini imefungwa mabao saba.

Vipigo ambavyo Ihefu ilivipata, vilisababisha uongozi wa timu hiyo kuamua kumtimua Kocha Mkuu, Maka Mwalwisi ambaye ndiye aliyeipandisha daraja wakidai kutoridhishwa na matokeo.

Kwa sasa Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama kupisha maandalizi ya Timu ya Taifa (Taifa Stars), Azam FC ndiyo timu vinara wa ligi hiyo wakiwa na pointi 15 wakati Ihefu yenye pointi tatu ni ya 17 huku Mbeya City inaburuza mkia ikiwa na pointi moja.




Mshindi wa bonasi ya Jackpot ya SportPesa, Patrick Metusela wa jijini Dodoma akiwa ameshika hundi ya mfano ya Sh. milioni 25.8 kwa ajili ya zawadi baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya mechi za mpira wa miguu wiki iliyopita. Jackpot ya SportPesa wiki hii ni Sh. milioni 225.1/-. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbeya City yakataa kumtimua Amri

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mbeya City imesema itaendelea na kocha wake, Amri Said na wala haifanyi kazi kwa kufuata mkumbo wa timu zingine ambazo zimetimua makocha.

Katibu Mkuu wa Mbeya City, Emmanuel Kimbe alisema wao wanaiheshimuwa taaluma ya ukocha na kwamba mpaka sasa hawajaona sababu yoyote ya kumtimua kocha huyo kwa sababu yeye si sababu ya timu hiyo kufanya vibaya.

"Hii siyo klabu ya mitaani, ina Bodi ya Wakurugenzi, kama kuna haja ya hilo basi bodi itakaa na kutazama mapana na marefu kuhusu jambo hilo na si kukurupuka, au tu kwa sababu Yanga na Ihefu zimefukuza kocha basi na sisi tufanye hivyo, hilo halipo," alisema Kimbe.

Kiongozi huyo alisema wao bado wana imani na Amri na kwamba kutofanya vema kwa Mbeya City kunatokana na sababu za kisayansi ya soka na wala si uwezo wa kocha au wachezaji.

"Sisi ndiyo timu ambayo tulicheza hadi kwenye mechi za mchujo, wakati wenzetu wakiwa wamemaliza ligi, hatukuwa na muda mrefu wa usajili na wala maandalizi ya msimu mpya kama wenzetu, kwa hiyo huwezi kusema eti kocha ndiyo tatizo," alisema kiongozi huyo.

Mbeya City mpaka sasa inakamata mkia ikiwa na pointi moja tu kwa mechi tano ilizocheza, ikitoka sare moja na kufungwa mechi nne, ikiwa ndiyo timu pekee kwenye ligi ikiwa haijafunga goli hata moja.

Hivi karibuni klabu za Yanga na Ihefu zimetimua makocha wao, Yanga ikimwondoa, Zlatco Krmpotic kwa kile kilichoelezwa kuwa timu haichezi vizuri huku Ihefu ikitangaza kuachana na Maka Mwalwisi kutokana na matokeo mabaya ya timu hiyo.

## Kayuni kuwanoa makocha Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), linatarajia kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa ajili ya makocha wenye leseni zinazotambulika na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), ili kuwajengea uwezo zaidi kuelekea katika msimu mpya.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa Ufundi wa ZFF, Ali Vuai Shein, alisema mafunzo hayo yanatarajia kufanyika kabla ya kuanza msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar kwa lengo la kuwapiga msasa makocha wote ili kuzitumikia vyema klabu zao.

Shein alisema mafunzo hayo yatakuwa kwa muda wa siku nne na yatashirikisha makocha kutoka Unguja na Pemba, huku yakitarajiwa kuendeshwa na Mkufunzi wa CAF, Sunday Kayuni kutoka jijini Dar es Salaam.

Kiongozi huyo amewataka makocha wote wenye sifa kuthibitisha ushiriki wao katika mafunzo hayo ili kutoa nafasi ya ZFF kukamilisha maandalizi ya kozi hiyo.

"Makocha wawe na mwamko wa kushiriki mafunzo mbalimbali yanayoandaliwa ndani na nje ya Zanzibar, mpira wa sasa hivi unategemea zaidi elimu kuliko mazoea, na mwalimu mzuri lazima apende kujifunza kupitia mafunzo mbalimbali, naomba watumie fursa hizi za masomo kwa kujiendeleza wao wenyewe," Shein alisema.

Aliwataka makocha wote wenye leseni hizo kushiriki mafunzo hayo muhimu kwa ajili ya kuanza msimu mpya kwa mafanikio.

## Mbio za Nyerere kufanyika Arusha

**Na Saada Akida**

MASHINDANO ya mbio za pikipiki maarufu Lakilaki kwa ajili ya kumwenzi Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere yamepangwa kufanyika Oktoba 17, mwaka huu jijini Arusha, imeelezwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano hayo, Ibrahim Salim, aliliambia gazeti hili mchakato wa kuandaa michuano hiyo umeshaanza na wanaamini idadi ya washiriki mwaka huu itaongezeka.

Salim alisema mashindano ya mwaka huu yatashirikisha wadau kutoka mikoa mbalimbali ya hapa nchini tofauti na miaka iliyopita walipokuwa wakishirikisha wenyeji pekee.

"Tumeshaanza maandalizi, ila mwaka huu tutakuwa tofauti, tumepanga kufanya mashindano Arusha, lakini tutapokea washirikishi kutoka mikoa mingine na nchi jirani ili kuipa heshima zaidi," alisema Salim.

Kiongozi huyo alisema pia wanatarajia kushirikisha baadhi ya madereva wa bodaboda, ili kupata madereva ambao watasaidia kwenye mchakato wa kuanzisha na kuendeleza chama cha mchezo huo mpya.

"Nimekuwa na utamaduni wa kila mwaka kuandaa mashindano haya ya pikipiki kwa ajili ya kumuenzi Baba wa Taifa, lakini tumekuwa na kampeni yetu ya uendeshaji salama wa chombo hicho ndio maana tunawashirikisha baadhi ya madereva bodaboda," Salim aliongeza.

Alieleza tayari wameshawasiliana na mamlaka husika, ili kusajili chama ambacho kitakuwa na mwongozo wa kalenda ya michuano yake mbalimbali.

Michezo
Ijumaa Oktoba 9, 2020
Nipashe



GIROUD AKARIBIA REKODI YA HENRY HABARI UK 22

# YANGA YAONGEZA 'DOZI' YA MAZOEZI

●●●Mwambusi afunguka bado wanahitaji kasi ili kuhimili ushindani uliopo katika mechi za Ligi Kuu...

**Na Saada Akida**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama kupisha kalenda ya kimataifa ya FIFA, benchi la ufundi la Yanga limeamua kuongeza programu ya mazoezi kwa lengo la kuimarisha wachezaji wake na hatimaye kutwaa taji la ligi hiyo ambalo linashikiliwa na watani zao.

Yanga itashuka tena dimbani Oktoba 22, mwaka huu kuwakaribisha 'Maafande' wa Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Msaaidizi wa Yanga, Juma Mwambusi, alisema amelazimika kuongeza muda wa kufanya mazoezi kwa sababu anahitaji kuona wachezaji wote wanakuwa fiti na tayari kucheza kwa dakika 90.

Mwambusi alisema licha ya kutopoteza mechi yoyote ya ligi katika raundi tano walizocheza, bado nyota wao hakuwa imara kama inavyotakiwa wakati msimu mpya unaanza.

"Tulikuwa tunafanya mazoezi mara moja, lakini sasa tutafanya mara tatu kwa siku, hii ni kwa ajili ya kukijenga kikosi kuwa fiti zaidi ili kufanya vizuri katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zinazofuata, tunataka kuwa na kikosi kilichoimarika," alisema Mwambusi.

Kocha huyo alisema msimu huu umekuwa na ushindani zaidi tofauti na hali aliyokutana nayo miaka ya nyuma alipokuwa na timu nyingine kwenye ligi hiyo inayoshirikisha timu 18 kutoka mikoa mbalimbali.

"Msimu huu ni mgumu zaidi kuliko kipindi chote ambacho nimewahi kufundisha timu Ligi Kuu, ligi imekuwa na ushindani mkubwa hali iliyosababisha nibadilishe programu ya mazoezi, sasa hivi tutafanya mazoezi mara mbili hadi tatu kwa siku," alisema kocha huyo.

Aliongeza mpira wa sasa ni sayansi na wanahitaji kujipanga vizuri kwa lengo la kuhakikisha wachezaji wanaimarika na kufikia kwenye kiwango anachokihitaji.

"Sio kila siku tutafanya mazoezi mara tatu, inategemea na siku kulingana na programu, sababu kubwa ni kutopata muda wa kutosha wa kufanya maandalizi ya msimu mpya, wachezaji wengi wao ni wapya, hivyo hawakupata muda wa kukaa pamoja na kuzoeana uwanjani, muda huu wa kalenda ya FIFA ndio muafaka wa kufanya mazoezi ya nguvu na kuendelea pale tulipoishia.

"Huu sio muda wa kupumzika au kulala, tunatakiwa kupiga kazi kuhakikisha wachezaji wote wanakuwa fiti na tayari kwa ajili ya michezo iliyopo mbele yetu bila kujali tunakutana na timu gani," alisema Mwambusi.

Aliongeza mbali na mazoezi ya uwanjani, pia amekuwa na ratiba ya kuzungumza na wachezaji wao kwa kuwakumbusha mambo muhimu wanayotakiwa kuyazingatia ili kufikia malengo yanayotarajiwa na viongozi pamoja na wanachama wa klabu hiyo.

Alieleza katika kuendelea kujiimarisha, kikosi chake kitacheza mechi ya kirafiki dhidi ya Mwadui FC kutoka Shinyanga itakayochezwa leo usiku kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini.

Yanga yenye pointi 13, iko katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kushinda mechi nne na kupata sare moja.




Mshambuliaji wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Thomas Ulimwengu (kushoto), akijaribu kumiliki mpira katika mazoezi ya timu hiyo inayojiandaa na mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Burundi itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam. Kulia ni nahodha wa timu hiyo, Mbwana Samatta. **PICHA: JUMANNE JUMA**


## BOCCO RASMI KUIKOSA BURUNDI

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) na Simba, John Bocco, ataukosa mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Burundi unaotarajiwa kufanyika Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.

Bocco aliumia katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya klabu yake dhidi ya Mtibwa Sugar na hivyo amekaa nje katika mechi mbili zilizopita za mabingwa hao watetezi dhidi ya Gwambina FC, Biashara United na JKT Tanzania.

Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije, alisema mshambuliaji huyo bado ni majeruhi na amemwondoa katika mipango ya mechi hiyo ya kirafiki na



kuongeza kukosekana kwake hakutaathiri mikakati ya kusaka ushindi.

Ndayiragije alisema ameshaandaa wachezaji watakaoziba nafasi hiyo na wamejiandaa vizuri kuwakabili wapinzani wao, huku akitarajia kupata ushindani mkubwa sababu ya makocha hao kufahamiana.

"Mechi itakuwa nzuri sababu tumejiandaa kufanya vizuri, lakini wenzetu nao wamejiandaa, kuhusu kukosekana kwa Bocco hakutaathiri mipango yangu ya mechi yetu ya Jumapili," alisema Ndayiragije.

Alimtaja kiungo, Himid Mao alitarajiwa kuwasili nchini jana usiku na leo ataungana na wenzake katika mazoezi ya timu hiyo.

"Burundi ni kipimo sahihi kwetu, sababu aina ya uchezaji hauna tofauti na wapinzani wetu Tunisia ambao tunatarajia kukutana nao Novemba 13, mwaka huu," kocha huyo alisema.

Taifa Stars imepangwa Kundi J katika kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika ikiwa pamoja na Tunisia, Equatorial Guinea na Libya.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002